epaper.ippmedia.com
www.ippmedia.com
0745 700710
LIKE & FOLLOW US

# Nipashe

Jumatatu Machi 25, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
MWANGA WA JAMII
ISSN 0856 • Na. 0581626
www.ippmedia.com
nipasheTZ nipasheTZ The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital



## ARAUJO ANAKANUSHA KUONDOKA BARCELONA

UKURASA 22

UCHAGUZI WA MARUDIO

# Vigogo NEC washinikizwa kuachia ngazi

UKURASA 2

UKURASA WA 8

### PROF. WANGWE: UCHUMI WA NCHI UNAKUA, LAKINI WANANCHI BADO MASKINI



MTAALAMU wa Uchumi, Prof. Samuel Wangwe amesema uchumi wa Tanzania unakua, lakini bado kuna umaskini...

UKURASA WA 21

### KANE SASA AREJESHWE RASMI BAYERN KUTIBIWA



MSHAMBULIAJI wa England, Harry Kane, amerudishwa Bayern Munich ili kuendelea...

## Jengo ICU lililogharimu mil. 280/- lavuja kabla ya kuanza kutumika

UKURASA 2




Paroko wa Parokia ya Mtakatifu Petro - Swaswa jijini Dodoma, Antipas Shayo, akiongoza waumini kwenye Ibada ya Dominika ya Matawi jijini humo jana. **PICHA: DORA TESHA**

**Ripoti** ya uchunguzi hali ya uchumi wa vyombo vya habari yaiva, kutua Ikulu

UKURASA 5



**Mongela** ataka mgombea mmoja nafasi ya urais

UKURASA 19

MAKALA MAALUM

## Kasi ya ongezeko la wajane yashtua, hadhari yatolewa

UKURASA 4

**MICHEZO** SIMBA, YANGA KAMILI KWA ROBO FAINALI CAF UK.24

**KATUNI** UK.6

## HABARI KITAIFA



Wajumbe wa Bodi ya Ubunifu ya Shirika la Mawasiliano Duniani (ITU) baada ya kukamilisha kikao cha kwanza cha Bodi hiyo kilichoketi Geneva Uswisi. Tanzania inawakilishwa kwenye bodi hiyo na Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania TCRA Dk. Jabiri Bakari (wa tatu kushoto, mstari wa nyuma). Bodi hiyo inajadili na kuweka mikakati ya Ubunifu wa TEHAMA katika nchi mbalimbali Duniani ili kuhakikisha inatumika kutatua changamoto za jamii. **PICHA: MPIGAPICHA WETU.**

# Vigogo NEC washinikizwa kujiuzulu

**Na Halfani Chusi**

CHAMA cha ACT Wazalendo kimemtaka Mwenyekiti wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), Jaji Jacobs Mwambegele pamoja na wajumbe wake wajiuzulu katika nafasi zao ili kutoa nafasi ya kuundwa Tume Huru ya Uchaguzi itakayofanya kazi ya kusimamia uchaguzi bila kuwa na upendeleo wowote.

Makamu Mwenyekiti wa chama hicho, Isihaka Mchinjita alitoa kauli hiyo alipozungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana na kuzungumzia matukio yaliyojitokeza katika uchaguzi wa marudio wa kata 23 uliofanyika wiki iliyopita.

Mchinjita alisema ACT wazalendo imeguswa na kusikitishwa na mwenendo aliodai usioridhisha wa uchaguzi wa marudio uliofanyika mara sita tangu kuingia madarakani kwa uongozi wa serikali ya awamu ya sita mwaka 2021.

Alidai kuwa katika uchaguzi wote wa marudio uliofanyika, hakuna tofauti hata ya msingi katika kuendesha na kusimamia uchaguzi kulinganisha na Uchaguzi wa Serikali za Mitaa Mwaka 2019 na Uchaguzi Mkuu wa 2020 ambao viongozi wa serikali na Chama Cha Mapinduzi (CCM) mara kadhaa wamenukuliwa wakikiri haukuwa huru.

Alitolea mfano, Mchinjita alidai kuwa katika uchaguzi wa kata 23, NEC ilishindwa kufanya kazi yake kwa weledi na kusababisha karatasi za kupigia kura kuwa mikononi mwa wananchi kabla ya muda wa kupiga kura.

"Tume ya Taifa ya Uchaguzi, miongoni mwa udhaifu wake kwenye uchaguzi huu wa marudio ni kugawa karatasi za kupigia kura kwa makada wa... (alitaja jina la chama cha siasa) walizotumia kutumbukiza kwenye masanduku ya kura. Hili limefanyika kwenye kata zote zilizorudia uchaguzi," alidai Mchinjita.

Aliongeza kuwa jambo la kusikitisha ni kuona polisi wakishindwa kuchukua hatua za kuwadhibiti wahalifu na badala yake wakawakamata watu waliotoa taarifa ya uhalifu huo wakati wa upigaji kura.

"Jitihada za viongozi wa ACT Wazalendo kuripoti suala hilo kwa maofisa wa NEC hazikusaidia kitu kwani hakuna hatua yoyote iliyochukuliwa na hata katika maeneo tuliyopata matokeo ya ushindi, matokeo yalibadilishwa," alidai.

Alitaja maeneo waliyoadai matokeo yamebadilishwa kuwa ni katika kata za Kasingirima, Mkoa wa Kigoma, Kabwe mkoani Rukwa na Chipuputa mkoani Mtwara.

"Kwa vile muundo na utaratibu mpya umepitishwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano kupitia Muswada wa Sheria ya Tume ya Uchaguzi, tume ya sasa ijiuzulu yote kupisha kuundwa kwa tume mpya itayopatikana kwa utaratibu wa ushindani.

"Ni muda mwafaka kwa NEC kuwa na watumishi wake hadi katika ngazi ya halmashauri ili uchaguzi usisimamiwe na watumishi wa halmashauri ambao wengi ni makada wa Chama Cha Mapinduzi (CCM)," alidai.

Aliongeza kuwa ACT Wazalendo imejiridhisha kupitia uchaguzi huo kuwa licha ya kauli za kufungua ukurasa mpya zilizotolewa na viongozi wakuu wa kitaifa kusaka mwafaka wa kitaifa, uchaguzi huo unadhihirisha kauli hizo ni za viongozi pekee.

Kuhusu polisi, Mchinjita alidai wamekuwa wanasiasa zaidi kuliko watendaji kwa kuwa walishiriki kukamata watu waliokuwa wanawaonyesha uovu ambao ni wajibu wao kuuzuia.

"Polisi walitumia mabavu kukamata viongozi wa ACT Wazalendo. Tukio hili limefanyika Halmashauri ya Kigoma Ujiji kwenye Kata ya Kasingirima. Viongozi waliokamatwa kwa kuzuia kura feki zisidumbukizwe kwenye masanduku ni Abdul Nondo (Mwenyekiti wa Ngome ya Vijana Taifa, Karama Kaila (Mjumbe wa Kamati Kuu Kanda ya Magharibi), Alhaji Selemani Simba (Mwenyekiti wa Ngome ya Wazee Mkoa wa Kigoma), Alumbula Khalidi aliyekuwa Mgombea Udiwani Kata ya Kasingirima na wanachama Ntakije Ntanena na Khamis Mzungu," alidai.

Simu ya Mwenyekiti wa NEC, Jaji Mwambegele ilipopigiwa na mwandishi wa habari hizi kuzungumzia shikinikizo hilo la kujiuzulu, iliita pasi na kupokewa licha ya kupigiwa mara tatu jana saa 11 jioni.

Wakati ACT Wazalendo wakilalama kuwapo rafu katika uchaguzi huo, CCM kupitia Katibu wa Halmashauri Kuu Idara ya Oganaizesheni, Issa Haji Ussi, imesema kuwa kwa furaha inashukuru na kupongeza Watanzania kwa kuendelea kuiamini na kuipa ushindi wa kata zote 23 kwa wastani wa asilimia 89, ikifuatwa na ACT Wazalendo katika uchaguzi huo uliofanyika Machi 20, mwaka huu.

Kwa mujibu wa Ussi, ushindi huo umetokana na umoja na mshikamano ndani ya chama, uteuzi wa wagombea bora na kampeni za kistaarabu na kisayansi zilizowafikia wapigakura.

## Jengo ICU lililogharimu mil. 280/- lavuja kabla ya kuanza kutumika

**Na Beatrice Shayo**

MKUU wa Wilaya ya Kilosa, mkoani Morogoro, Shaka Hamdu Shaka, ameagiza kupatiwa taarifa ya mradi wa ujenzi wa jengo la wagonjwa wanaohitaji uangalizi maalum (ICU) lililogharimu Sh. milioni 278, lakini limebainika kuwa na matatizo mengi, ikiwamo kuvuja kabla ya kuanza kutumika.

Jengo hilo jipya limejengwa katika Hospitali ya Wilaya ya Kilosa, limeanza kukarabatiwa kabla ya matumizi, huku fundi wa kwanza hawajui aliko, hivyo wamelazimika kutafuta fundi mwingine.

Vilevile, fedha za mradi zimeisha, imewalazimu kuchukua fedha nyingine katika mfuko wa hospitali ili kufanya ukarabati huo katika jengo hilo.

Akizungumza na watumishi na viongozi wa hospitali hiyo baada kutembelea na kukagua jengo hilo kwa mara ya pili mwishoni mwa wiki, Shaka alisema mradi huo umejengwa chini ya kiwango na kuagiza kupatiwa taarifa ya mradi mzima.

Alisema mbali na kuvuja, pia kuna ufa, milango na paa havifai huku akiagiza marekebisho yafanyike.

"Fedha zimeletwa zaidi ya Sh. milioni 200 katika mradi huu lakini cha kusikitisha viongozi mmeshindwa kujitambua, umakini na kusimamia jukumu hili, pamoja na yote mnaniambia hata mjenzi wa awali mliyempa kazi na kuharibu hamjui mtampata wapi.

"Mambo ya ajabu sana, haiwezekani kabisa ndio maana ninataka vyombo vyote vya ulinzi na usalama vilivyopo hapa kila chombo kibebe jukumu lake.

"Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) mpo hapa, Jeshi la Polisi mpo hapa na vyombo vingine, kila mmoja afanye jukumu lake, itakapofika Jumatano ninataka taarifa tumechoka hizi hadithi ukienda ukirudi unapatiwa hadithi nyingine, msicheze na fedha za serikali," aliagiza.

Shaka pia alieleza kushangazwa na namna mradi huo ulivyotekelezwa kwa kutumia vifaa alivyoviita vya kuungaunga, visivyo na ubora, pia kuwekwa saruji katika paa la jengo kunakosababisha kuvuja.

"Ina maana huyu ameenda dukani kuomba vipande vipande vya mikanda ya gpsum ndio amekuja kutuwekea hapa, huwezi kusema hii mikanda imekuja kwenye jengo la serikali halafu kafanya hivi kwa jengo zima, viongozi mpo mnangalia, mnaona ni sawa, hapa pana tatizo," alisema Shaka akiahidi atakayebainika 'kucheza' katika uzembe huo atawajibishwa kwa mujibu wa sheria.

"Kama kuna kamati ama nani kahusika na huu uzembe, kila mmoja akajitathmini mapema; anatosha kwenye dhamana aliyopewa, vinginevyo sina msalie mtume, mradi huu tunauweka chini ya uangalizi kuanzia sasa tunaunda kamati ndogo itakayosimamia ujenzi, ukarabati na marekebisho mpaka yakamilike.

"Nilikuja mara ya kwanza nikatoa maelekezo, leo mnaniletea hadithi mpya, hapana, hapana, hapana! Hatutaki maneno, tunataka huduma kwa wananchi," alisema Shaka.

Mganga Mkuu wa Wilaya ya Kilosa, Saimon Swai alisema: "Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya, tukiri upungufu huu, ni kweli tulipokea maelekezo yako, lakini mimi si msemaji sana, ila tulimtafuta fundi aliyepewa kazi tukamkosa. Hatukumpata na tukalazimika kutafuta fundi mwingine ambaye ndiye huyu anaendelea na kazi kwa kutumia fedha za hospitali baada za awali kuisha."


## NOTISI/TANGAZO

**LEGENDS AUCTION MART LTD, DESTENI COMPANY LIMITED, NUTMEG AUCTIONEERS & PROPERTY MANAGERS CO.LTD ,SALEI AUCTION MART LTD,HEDANE ENTERPRISES LTD, MASE INTERNATIONAL LTD,TAUSI AUCTION MART,MASETO AUCTIONEER AND DEBT COLLECTORS, JY AUCTIONEERS CO.LTD,DRM AUCTIONEERS & CO.LTD, MAS AND ASSOCIATES CO.LTD,MELVA INTERNATIONAL LTD ,SUMA JKT AUCTION MART COMPANY LTD,MAJEMBE AUCTION MART LTD, MABUNDA AUCTIONEER MART CO.LTD, TRUST RECOVERIES LTD, BEST GROUP (T) LTD,JAMOK INVESTMENT LTD,MCHINGA AUCTION MART,GADAU AUCTION MART,AMI AUCTION MART, IGALULA AUCTION MART,BAHARI AUCTION MART, ADILI AUCTION MART,KOTI BROTHERS CO. LTD,PROPERTY MASTER LTD,MULTLINK AGENCY LTD,TWINS AUCTIONS MART, BID CITY AUCTION,jJALAS AUCTION MART,HOLLYNESS COMPANY LTD** kwa mamlaka tuliyopewa na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, chini ya **AKIBA COMMERCIAL BANK PLC,** tunatoa notisi ya kulipa deni kwa mdaiwa ndani ya siku 14 kuanzia tangazo hili, Vinginevyo, tutafanya Minada ya hadhara kama ratiba inavyoonyesha.

| TAWI ALILOKOPA | JINA LA MTEJA | AINA YA DHAMANA | JINA LA MWENYE DHAMANA | MAHALI DHAMANA ILIPO | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|---|---|
| MBAGALA | NORBERT LUDOVICK KWIYAKA | NYUMBA | NORBERT LUDOVICK KWIYAKA | CHAMAZI DOVYA | 08/04/2024 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MBEYA | KIVAULA MLIMKA LUHANGA | NYUMBA (2) ZENYE HATI MILIKI | KIVAULA MLIMKA LUHANGA | 1.MBEYA MJINI 2. TUNDUMA | 26/03/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |

**MASHARTI YA MNADA**

1 Mnunuzi atalazimika kulipa 25% ya bei ya Nyumba, Kiwanja, Gari au Shamba ,papo hapo baada ya mnada kumalizika na 75% itakayobaki italazimika kulipwa ndani ya siku 14.
2 Ikiwa mnunuzi atashindwa kutimiza sharti lolote la mnada kuhusiana na malipo ya awali,hatarudishiwa pesa yoyote aliyokwisha ilipa.
3 Kwa mawasiliano zaidi; tupigie simu no.**0714939933/0715868000**
4 Iwapo ndani ya siku 60 mnunuzi hajakabidhiwa nyumba Benki itarudisha kiasi cha fedha kilichowekwa na mnunuzi Benki bila gharama yeyote.

217892402

## HABARI KITAIFA



# Kasi ya ongezeko la wajane yashtua

## -Chama cha Wajane chatoa hadhari, chaanza kufanya utafiti kiini vifo vingi vya wanaume...

Na Romana Mallya

WAJANE wanaongezeka kwa kasi nchini, Chama cha Wanawake Wajane Tanzania (CCWWT) kimebainisha.

Katika mazungumzo na mwandishi wa habari hizi, Katibu wa chama hicho, Sabrina Tenganamba amesema amebaini kuwapo kasi ya ongezeko la wajane, hali aliyoitafsiri ni ishara ya kuwapo vifo vingi vya wanaume nchini.

Sabrina anasema wameanza utafiti kubaini kiini cha vifo vingi vya wanaume; kwanini kesi za mirathi zinakaa muda mrefu mahakamani na kwanini wajane wanashindwa kujisimamia wenyewe kiuchumi.

Licha ya kushika nafasi ya sita nchini kwa kuwa na idadi kubwa ya watu, ukiwa na watu 2,989,299, Sabrina anautaja Mkoa wa Kagera kuongoza kuwa na wajane wengi walio katika chama hicho.

Matokeo ya Sensa ya Watu na Makazi 2022 yanaonesha Kagera inazidiwa kwa idadi ya watu na mikoa ya Dar es Salaam (5,383,728), Tabora (3,391,679), Mwanza (3,699,872), Morogoro (3,197,104) na Dodoma (3,085,625).

Katika mazungumzo na Nipashe,

Sabrina anabainisha kuwa Mkoa wa Kagera una wanachama wengi wanaofikia 32,000 kati ya 148,000 wenye kadi maalum za chama chao katika mikoa 16 nchini.

**KULIKONI KAGERA?**

Sabrina anasema kuna sababu nyingi zinazochangia changamoto hiyo mkoani Kagera, akiutaja umekumbwa na madhila mengi kama magonjwa ya kuambukiza ukiwamo Upungufu wa Kinga Mwilini (UKIMWI); Virusi vya UKIMWI (VVU) viliingia nchini kupitia mkoa huo na ndioülioathirika zaidi.

Kuhusu vifo vitokanavyo na UKIMWI kuwa vingi zaidi kwa wanaume kuliko wanawake, Mratibu wa Kudhibiti UKIMWI Mkoa wa Manyara, Dk. Charles Shija, anasema wanaume wanaongoza kwa vifo vitokanavyo na UKIMWI kulinganisha na wanawake kwa sababu si wepesi wa kutaka kujua hali zao kiafya, hivyo wanapofika hospitalini au kituo cha afya hujikuta virusi vimeshaingia kwenye hatua ya pili.

"Kwahiyo, wanaume wengi hugundulika kipindi ambacho virusi vimeingia katika hatua ya UKIMWI. Ndio maana wanawake wanaongoza kwa maambukizi ya VVU, lakini wanaume wanaongoza kwa vifo vitokanavyo na UKIMWI," anasema.

Ni hoja inayoungwa mkono na Nyangusi Laiser, Ofisa Ufuatiliaji na Tathmini wa Tume ya Taifa ya Kudhibiti UKIMWI (TACAIDS), anayebainisha kwamba, mwaka 2020 Tanzania ilikuwa na maambukizi mapya ya VVU kwa watu 68,000. Kati yao 37,000 ni wanawake (asilimia 54.4) na wanaume 21,000.

Vilevile, Meneja Mfuko wa Udhamini wa Kudhibiti UKIMWI Tanzania (ATF), Peter Kivugo, alikaririwa na Nipashe mwaka juzi akisema, "Vifo vitokanavyo na magonjwa nyemelezi kwa wanawake vimepungua, lakini kwa wanaume vinapanda.

"Wengi wanakufa mapema kutokana na kushindwa kuzingatia maelekezo ya dawa na kujizuia katika tabia hatarishi ambazo zinasababisha kupata maambukizi mapya na magonjwa mengine ya zinaa," alisema.

Kivugo alirejea takwimu za vifo vitokanavyo na UKIMWI kwa mwaka 2019, akibainisha vilikuwa 21,526 kwa watu wenye umri kuanzia miaka 15, wanaume wakiwa 12,225 (asilimia 56.8) na wanaume 9,304 huku watoto chini ya miaka 15 vilikuwa 5,900 na hivyo kufanya jumla ya vifo 27,429.

Unaporejewa ufafanuzi wa Katibu wa CCWWT, Sabrina, mbali na changamoyo ya VVU na UKIMWI, Mkoa wa Kagera pia unakabiliwa na changamoto za mila na desturi ambazo zinamweka hatarini zaidi mwanamume kulinganisha na mwanamke, ikiwamo kurithi wajane.

Sabrina anataja mikoa mingine yenye wanachama wengi wajane ni Iringa (29,000) na Mbeya (27,000).

**UTAFITI WAANZA**

Sabrina anasema kutokana na changamoto wanazopitia wajane, wameamua kufanya utafiti ili kila wanapokwenda mikoani kwa wanachama wao, wawe na majibu mkononi kuwahusu na kuzitafutia ufumbuzi.

"Utafiti tulianza mwaka 2022, unalenga mambo matatu; Kwanza, tumebaini wajane wanazidi kuongezeka hivyo, tunafanya utafiti kwanini wanaume wanakufa sana.



Baadhi ya wanachama wa Chama cha Wajane wakimsikiliza Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia,Wanawake na Makundi Maalum, Dk Doroth Gwajima wakati akizindua chama hicho tawi la Dar es Salaam. **PICHA: MTANDAO**

> **"Tusije kushangaa wanawake tukabaki peke yetu duniani, tukibaki peke yetu itakuwa kituko".**

"Takwimu tunazozitaja kichama ni za wanachama hai wenye kadi, lakini wapo wengi katika mikoa mbalimbali ambao huwa tunakwenda na bado hawajajiunga nasi. Tusije kushangaa (wanawake) tukabaki peke yetu duniani, tukibaki peke yetu itakuwa kituko.

"Utafiti wa pili tunaofanya ni kwanini kesi za mirathi zinakaa muda mrefu mahakamani na wa tatu ni kwanini wajane wanashindwa kujisimamia wenyewe kiuchumi? Hii inatokana na kesi nyingi tunazozipata kwa wanachama wetu.

"Utafiti huu unahusisha wadau mbalimbali wakiwamo wenye mamlaka husika, lengo ni kuja na suluhu ya changamoto zinazotukabili wajane. Tunatambua waathirika wakubwa ni watoto na kama nilivyoesma, kuna shida inapaswa kutafutwa ufumbuzi wanaume wengi wanakufa," alisema. Sabrina anataja changamoto nyingine ambazo wajane wanapitia ni pindi wanapoachwa bila chochote, hujikuta wanaingia katika mikopo ya kausha damu na matokeo yake badala ya kubadilisha maisha, wanakuwa watumwa wa taasisi zinazotoa mikopo.

"Matokeo yake wanaishia kupata sonona na kufariki dunia. Tumezika wajane sita kwa sababu ya mikopo ya aina hii. Walikopa ili kuendesha maisha, wakashindwa kurejesha, baadhi wakapata sonona, wakafariki dunia.

"Mwaka 2023, walijinyonga wanachama wetu wawili kwa sababu ya madeni, ni wanachama wetu kutoka Iringa na Sumbawanga.

"Huko Geita, kuna mjane mwanachama wetu alichinjwa kwa panga na mtoto wake, akidai mama yake ni mchawi, akimtuhumu kuwa amemuua baba yake na mtoto wake (mjukuu) kwa hali ya kuhisiwa tu kwamba ukifiwa na mume umeua, na watoto wanapandikizwa chuki mama ni muuaji," anasema.

**JAMII INAWACHUKULIAJE?**

Sabrina anasema kwa sasa jamii imeanza kuwaelewa, lakini miaka ya nyuma waliwachukulia kama wanajitangaza kuwa wapo 'single' ili kupata wanaume.

"Hata sherehe tunayoifanya Juni 23, kila mwaka, wengi ndani ya jamii wanasema tunasherehekea kufiwa na waume zetu. Lakini, siku hii kwetu imelenga mjane kutengenezewa ufahamu upya na kumfariji kwa kuwa ndiye anayelea watoto yatima.

"Siku hii tunakutana na marafiki wapya. Unaweza kuwa kwako unaona upweke na kulia, lakini ukitoka na kuchangamana na wengine unakutana na shuhuda za kukutia moyo.

"Wapo waliofanikiwa wamesomesha watoto wao mpaka chuo kikuu, mwingine anashuhudia ameshinda kesi yake. Unapokutana na shuhuda hizi zinakutia moyo kuanza upya na kutengeneza ufahamu upya," anasema.

**HISTORIA YA CHAMA**

Sabrina anasema chama hicho kilianza mwaka 2014 kwa wajane kukutana na kutiana moyo kwa yale yanayowakabili na kusaidiana kwa kuwachangia wasio na mitaji ili kuanzisha biashara ndogo.

Anasema waliweka utaratibu kwa wanaoingia katika chama bila ya kuwa na mwelekeo wa maisha kutokana na historia zao za kuwategemea waume zao kwa asilimia 100 kiuchumi, wanafundishwa namna ya kujikwamua ili kuendeleza familia walizoachiwa.

"Januari 18, 2021, chama kilipata usajili rasmi. Tulipoanza tulikuwa wajane 12, lakini sasa (2024) tumefikia jumla ya wajane 148,000.

"Hawa ni wanachama wenye kadi maalum za chama wanaotoka mikoa ya Dar es Salaam, Katavi, Tabora, Lindi, Mtwara, Pwani, Kagera, Dodoma, Njombe, Songwe, Mbeya, Iringa, Tabora, Geita, Shinyanga na Rukwa.

**TAKWIMU TRAFIKI**

Wakati utafiti ukianza kubaini sababu za waume kufa mapema, takwimu za Jeshi la Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani nchini, zinaonesha kuwa kipindi cha kuanzia Januari hadi Desemba 12, 2023, kilikuwa na ajali za barabarani 1,641 zilizotokea na kusababisha vifo vya watu 1,550. Kati ya hao, wanaume ni 1,189 na wanawake ni 391.

Ajali hizo zimesababisha majeraha kwa watu 2,562. Kati yao, wanaume ni 1,721 na wanawake ni 841.

Vilevile, Msaikolojia Tiba, Geofrey Mwamnyanyi anayefanya kazi na shirika la lisilo la kiserikali Initiative of Change, alikariri na Nipashe mwaka 2022, akisema zipo sababu nyingi za vifo kwa wanaume ikiwamo mfumo wa mwili na za saikolojia.

Alisema wanaume wanawahi kufa kutokana na sehemu wanazotokea kibailojia au asili ya kuumbika kwao kufungwa seli ambazo hazina uhai kwa muda mrefu, akidokeza kuwa wanaume wengi huishi miaka mitano nyuma ya mwanamke.

Alisema sababu za kisaikolojia zinaathiri mfumo wa maumbile ambapo wanaume wameumbwa na nguvu ya kufanya uamuzi, akifafanua, "Uwezo wa mwanamume kutafakari mambo upo kwenye misuli mikubwa zaidi kuliko mwanamke. Mwanamume hana nguvu kubwa kwenye kutafakari mambo, yeye yupo kwenye hatua ya kufikia hitimisho la jambo."

Mtaalamu huyo alitaja mila na tamaduni za Kiafrika zinamfanya mwanamume afe mapema kwa kuwa zinamfanya awe ndiye mtoaji wa vitu vyote kuhakikisha anapambana ili asipate aibu.

"Wanaume wengi wanashindwa kujizuia kwenye kupata tendo la ndoa na hawazingatii ulaji ili kufanya kazi kwenye ubora wa kuzalisha madini mengine, wanajikuta virutubisho vingi wanapoteza katika tendo la ndoa kuliko ambavyo wanaingiza," alionya.

**ITAENDELEA KESHO**

## HABARI KITAIFA



Rais wa Klabu ya Rotary ya Dar es Salaam, Nikki Aggarwal (aliyeshika mche wa mti), akishirikiana na wanachama wa klabu hiyo kupanda miti katika msitu wa Kazimzumbwi, Kisarawe mkoani Pwani, mwishoni mwa wiki. Rotary inapanda miti 2,500 ikiwa ni sehemu ya kampeni yake ya kutunza mazingira sambamba na utoaji wa madawati kwa shule za msingi ambapo imetoa madawati takriban 4,000 yenye thamani ya shilingi milioni 500 na kuwanufaisha wanafunzi zaidi ya 10,000. **MPIGAPICHA WETU**

# Ripoti kamati kutathmini uchumi wa vyombo vya habari kutua kwa Rais

**Na Elizabeth Zaya**

RIPOTI ya Kamati iliyoundwa kwa ajili ya kutathmini hali ya utendaji na uchumi kwenye vyombo vya habari inatarajiwa kukabidhiwa hivi karibuni kwa Rais Samia Suluhu Hassan.

Akizungumza na wahariri wa vyombo vya habari jijini Dar es Salaam jana kuhusu miaka mitatu ya Rais Samia madarakani ambayo iligusa sekta mbalimbali nchini, Msemaji Mkuu wa Serikali, Mobhare Matinyi, alisema kamati ilikamilisha kazi hiyo Januari, mwaka huu.

"Kufuatia maelekezo ya Rais Samia, aliyoyatoa mwaka jana, Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye, aliteua kamati ya kutathmini hali ya utendaji na uchumi kwenye vyombo vya habari na kuelekeza kuwa dhamira ya serikali ni kushughulikia suala la uchumi kwa vyombo vya habari. Kamati hiyo imeshakamilisha kazi hiyo na taarifa yake inatarajiwa kuwasilishwa kwa Rais kwa ajili ya maelekezo yake," alisema Matinyi.

Alisema kamati hiyo imewasilisha taarifa hiyo kwa Waziri Nape na kwamba hatua iliyobaki ni kufikisha kwa Rais Samia kusubiri maelekezo.

"Tayari kamati imeshawasilisha ripoti yake kwa waziri na hatua iliyobaki ni kufikisha kwa Rais Samia na kusubiri maelekezo yake ya namna gani serikali inatakiwa kutoa ushirikiano wa kuikomboa sekta ya habari hapa nchini kutokana na hali ngumu inayovikabili vyombo hivyo kutokana na teknolojia ambayo imehamishia vitu vingi kwenye mitandao na changamoto zilizoibuka wakati wa UVIKO-19," alisema Matinyi.

Kamati hiyo ya watu tisa iliyoteuliwa na Waziri Nape kwa maelekezo ya Rais Samia, awali ilipewa miezi mitatu kukamilisha kazi hiyo, lakini baadaye iliongezewa muda na kutakiwa kuikamilisha ndani ya miezi sita.

Kuhusu uchumi, fedha na uwekezaji, Matinyi alisema Tanzania imeendelea kuwa kasiliana kundi la nchi zenye uchumi wa pato la kati, ikimaanisha pato la wastani la kila mwananchi kwa mwaka (GNI per capita) ingawa mwaka 2019 ilikuwa ni dola 1,080 za Kimarekani, lakini mwaka 2022 ni dola 1,200.

Alisema serikali pia imeendelea kudhibiti mfumuko wa bei na kwa sasa ni chini ya asilimia nne

ambacho ni miongoni mwa viwango bora katika nchi za jumuiya za kikanda ambazo Tanzania ni mwanachama, kama Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) na Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC).

Kuhusu Ofisi ya Msajili wa Hazina, alisema thamani ya uwekezaji katika taasisi zinazosimamiwa na ofisi hiyo imeongezeka kutoka Sh. trilioni 70 mwaka 2021 hadi kufikia Sh. trilioni 76 mwaka 2023 sawa na ongezeko la asilimia 8.6.

"Sababu ya ongezeko hili ni serikali ya awamu ya sita kuongeza mitaji kwa Sh. trilioni 5.5 katika mashirika ya kimkakati kwa maslahi ya taifa. Ofisi pia imeongeza makusanyo ya mapato yasiyo ya kodi kutoka Sh. bilioni 637.66 hadi trilioni 1.008 kwa mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 58.

Serikali pia imeongeza umiliki wa hisa katika kampuni ya almasi ya Williamson Diamonds kutoka asilimia 25 hadi 37 huku ikisaini mikataba ya ubia wa asilimia 16 zisizohamishika katika kampuni za madini.

Kwenye sekta ya kilimo, alisema bajeti imeongezeka kutoka Sh. bilioni 294.16 mwaka 2021/2022 hadi kufikia Sh. bilioni 970.78 mwaka wa fedha 2023/2024.

"Matumizi ya mbolea yameongezeka kutoka tani 320,233 kwa mwaka wa fedha 2020/21 hadi kufikia tani 580,628 kwa mwaka wa fedha 2022/23," alisema.

Katika kipindi cha miaka mitatu 2021/22 hadi mwaka 2023/24, bajeti ya sekta ya mifugo imekua ikiongezeka kwa kasi. Bajeti hiyo imeongezeka kutoka Sh. 47,844,950,000 mwaka 2021/22 hadi Sh.112,046,777,000 mwaka 2023/24.

Aidha, Matinyi alisema sekta ya uvuvi katika kipindi cha miaka mitatu, 2021/22 hadi mwaka 2023/24, bajeti ya sekta ya uvuvi imependa kutoka Sh.121,350,046,999 mwaka 2021/22 hadi Sh. 183,874,156,000 mwaka 2023/24.

# Elimu afya uzazi yatajwa mkombozi kwa wasichana

**Na Mwandishi Wetu**

KUNA haja kuendelea kutoa elimu ya afya ya uzazi kwa wasichana walio katika rika la kubalehe ili kuwaepusha na tatizo la mimba zisizotarajiwa na wengine kuacha masomo. Ni rai ya wadau wa masuala ya jinsia wanaotaka mashirika na serikali kuendelea kutoa elimu ya afya ya jinsia katika jamii. Mkurugenzi Mtendaji na Mwanzilishi wa Binti Salha Foundation, Salha Azizi, akizungumza na wanafunzi wa Shule za Msingi za Mkoa wa Dar es Salaam juzi jijini, alisema kuna haja ya kutoa elimu hiyo kwa vijana hasa katika shule hizo ili kujenga jamii iliyo na afya bora.

"Kama ilivyo ada huwezi kumsubiri ng'ombe akue ndipo umnenepeshe, lazima uanze mapema, nasi lengo letu ni kutoa taarifa sahihi kwa watoto pamoja na walimu wao ili kuwajenga wangali wakiwa wadogo.

"Pia tumetoa elimu kwa watoto namna ya kujikinga dhidi ya ukatili ikiwamo masuala ya ubakaji na ulawiti," alisema mkurugenzi huyo. Aliwataka walimu kuendelea kujenga urafiki na wanafunzi ili wapate taarifa sahihi kuhusu masuala mbalimbali yanayowakabili ikiwamo ukatili wa kijinsia ili wazipatie ufumbuzi kwa wakati sahihi. Nesaa Mbwambo, Mwalimu wa Shule ya Msingi Ilala Boma, alisema walimu wamekuwa wanaelimisha wanafunzi kupitia elimu darasani na klabu walizonazo katika shule na kuwashukuru Salha Foundation, Msichana Initiative na wadau wengine kwa kuendeleza kutoa elimu hiyo maeneo mbalimbali nchini.

"Katika afya ya uzazi tunaanza na elimu ya balehe hasa kutambua jinsi ya kujihifadhi, matatizo yanayotokana na uzazi, njia za kujikinga na matatizo hayo ili waweze kuepuka madhara yanayoweza kujitokeza kutokana na ukosefu wa elimu ya uzazi," alisema mwalimu huyo.

Alieleza changamoto kubwa zinazowakumba watoto shuleni ni pamoja na mimba za utotoni na hata kuwasababishia vifo, akisisitiza mimba hizo ni zao la kukumbana na vishawishi njiani kutokana na umbali uliopo kuifikia shule na hali ya umaskini wa kaya, pia kukosa malezi bora na elimu ya afya ya uzazi.

Wanafunzi hao kutoka Shule za Msingi Ilala Boma, Msasani na Tandale walieleza madhara mbalimbali yanayoweza kujitokeza kutokana na ukosefu wa elimu ya kutosha ya afya ya uzazi na jinsia kwa wanafunzi walioko shuleni Elimu hiyo ilitolewa kwa pamoja na Shirika la Binti Salha Foundation, Msichana Initiative na WGNRR Afrika.

Ripoti ya Utafiti wa Afya ya Uzazi na Mtoto na Viasharia vya Malaria Tanzania ya Mwaka 2022, inaonesha kuwa pamoja na Tanzania kupunguza viwango vya mimba za utotoni kutoka asilimia 27 mwaka 2015/16 hadi asilimia 22 mwaka 2022, bado kuna maeneo yenye idadi kubwa ya watoto wanaokumbana na ukatili huo.

Ripoti inaitaja mikoa ya Dodoma, Kigoma, Tabora na Shinyanga imepunguza viwango vya mimba za utotoni kwa kasi kubwa zaidi kulinganishwa na mingine, huku Mkoa wa Dar es Salaam mimba za utotoni zikiongezeka kutoka asilimia 11.9 hadi asilimia 18.1. Mkoa huo pia unaongoza kwa idadi ya watu nchini.


CRDB BANK
*The bank that listens*

## PROVISION OF EMPLOYEE WELLNESS PROGRAM 2024-2026

**INTRODUCTION:**

CRDB Bank Plc would like to invite prospective proponents to submit proposals for the provision of Employee Wellness Program for 2024/2026.

**OBJECTIVES:**

The objective is to engage a qualified wellness Consultant who will partner with CRDB Bank in fostering a workplace culture of wellness to increase productivity and welfare of the employees.

**KEY FOCUS AREAS**

1. **Professional Telephone Counselling in Swahili and English** -
   Counselling for psychosocial problems, substance abuse and addiction, relationship problems, financial management, health, personal, or work-related problems and all mental disorders.
2. **Professional Face to Face Counselling** -
   For any psychological, relationship, medical, stress, financial problem, marital & pre-natal counselling, trauma focused counselling, teenage counselling, family therapy, individual and corporate coaching, fitness, nutrition, and lifestyle management.
3. **Managerial Consultation**
   Managerial consultancy for stress management, crisis management, assistance in managing risk cases, cultural diversity, or performance management of employees.
4. **Psychiatric Care Arrangement**
   Outpatient assessment and care through accredited Psychiatrist.
5. **Emergency Response Critical Incident Stress Debriefing (CISD)**
   Worksite Counseling and Stress Management Support such as armed robbery, death, or disaster at a worksite.
6. **Education Support and Awareness –**
   Conduct awareness program across the network to equip employees on key psychological threat / sign periodically.
7. **Home Based Care Services –**
   Support of home health services where needed.
8. **Physical wellness -**
   Support physical wellness that encourages the balance of physical activity, nutrition, good sleep, and mental well-being.
9. **Wellness Days** –
   Support in conducting annual wellness days across the network that helps to keep employees well educated in various health issues etc.
10. **Monitoring & Reporting –**
   Monthly, Quarterly & Annual
11. **Submission of Tenders -**
   All tender submissions must be online.
   Emails where tenders should be sent reads as below, any email sent sizes should be 4MB or less.
   - procurementdesk@crdbbank.co.tz
   - tenders@crdbbank.co.tz

   As part of the technical and financial evaluation of proposals, please indicate the following details in your proposal:
   i. Submit a Company Profile
   ii. Submit a detailed relevant experience with evidence attached, at least three (3) Contracts, LPO, Recommendation letters) including customers served before and type of work undertaken.
   iii. Submit at least three (3) Recommendation letters for customers served before and type of work undertaken.
   iv. Location of regional offices (HQ & Branches if Any)
   v. Annual reports / audited financial reports for the past three (3) years.
   vi. Current Annual return certificate, for Tanzania companies, this is obtained from BRELA.
   vii. Submit legal and business certificates.
   viii. Submit valid Regulatory, Government Board or Agency certificate required for such goods/services.
   ix. Submit Valid Business license.
   x. Employees CVs & certificates
   xi. The following forms are available in our website for filling and submitting as part of the requirements, vendor application, Non-disclosure agreement and Bank indemnity form.
12. **Deadline of submission to be indicated as**
   - Tender deadline for submission 05th April 2024
   - Tender Closing time 12:00 hrs
   - Tender opening time 16:00 hrs (a link will be sent through to the email that submitted the tender)

**The Managing Director**
CRDB Headquarters,
Plot No.25 & 26 Ally Hassan Mwinyi Road &
Plot No.21 Barrack Obama Road
P.O. Box 268, 11101 Dar es Salaam, Tanzania
Tel: +255 (0) 22 211 7441 – 7
Fax: +255 (0) 22 211 6714
Email: info@crdbbank.co.tz
Website: http://www.crdbbank.co.tz

217887202

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Simba, Yanga malizeni mechi CAF nyumbani

**IJUMAA** na Jumamosi wiki hii, ni siku zinazosubiriwa kwa hamu na Watanzania wengi wapenda michezo kwani timu zao kubwa na kongwe nchini, Simba na Yanga, zitashuka dimbani kucheza mechi za robo fainali za Ligi ya Mabingwa Afrika.

Ijumaa, Simba itashuka Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam kucheza dhidi ya Mabingwa Watetezi, Al Ahly ya Misri na Jumamosi, Yanga nayo itakuwa hapo hapo kuikaribisha Mamelodi Sundowns ya Afrika Kusini.

Baada ya mechi hizo, timu hizo zitalazimika kwenda ugenini kucheza michezo ya marudiano, Aprili 5, mwaka huu, Simba ikiwa Cairo nchini Misri na Yanga Afrika Kusini. Matokeo ya Jumla baada ya mechi hizo mbili kwa kila timu ndiyo yataamua timu zipi zitakwenda hatua ya nusu fainali. Kwa maana hiyo ili timu za Tanzania ziweze kusonga mbele hatua ya fainali zitatakiwa kupata ushindi mnono nyumbani ili kujiweka katika mazingira mazuri zinapokwenda ugenini.

Hatuna maana kuwa timu zetu haziwezi kutoka sare ugenini, au kushinda, la hasha, zimeshafanya hivyo sana, lakini kwa uzoefu wetu kwa soka la Kiafrika unaonyesha kuwa asilimia kubwa timu hushinda zinapocheza kwenye viwanja vyao vya nyumbani.

Hivyo, tunachotaka kuwaambia Simba na Yanga ni kwamba kama wapinzani wao wakiingia kwenye mfumo, basi wazimalize mechi hapa hapa na si kucheza lelemama.

Kama kuna uwezekano timu kufungwa mabao matatu, manne, sita hata saba, hazina budi kutumia nafasi hiyo kufanya hivyo bila huruma, au kucheza na jukwaa. Rai hii hasa ni kwa wachezaji wa Simba ambao huwa na tabia ya kuridhika na mabao machache wanayofunga na kuanza kuonyesha ufundi ili wasikie makelele jukwaani, jambo ambalo kwa mechi za hatua kama hii linapaswa kukemewa vikali.

Wakumbuke hizi ni mechi za maamuzi tu, na si za ligi au makundi. Ni mechi ambazo Al Ahly wanajua kuzicheza kwani wao hawataki mbwembwe, bali ni matokeo mazuri tu.

Kadhalika, wachezaji wa Simba na Yanga wanatakiwa wawe makini katika kutumia vizuri nafasi zinazopatikana kuweka mpira wavuni, kwani wakumbuke ni idadi kubwa ya mabao ndiyo itakayowasogeza karibu na hatua ya nusu fainali.

Katika mechi hizi, tunawaasa pia wachezaji wa timu hizo hasa mabeki kutokuwa na tabia ya kuchezacheza na mpira langoni. Kama kuna uwezekano wa kuuondoa kwenda mbali ondoa na si kupasiana nyuma bila sababu ya msingi, kwani hilo linatakiwa kufanyika dakika za mwisho tena timu ikiwa na ushindi mnono mkononi.


Tunayasema hayo kwa sababu katika mechi kama hizi kuruhusu bao nyumbani linaweza kuigharimu timu kwenye mechi za marudiano kwani Shirikisho la Soka Afrika bado linatumia kanuni ya faida ya bao la ugenini pale timu mbili zinapolingana kila kitu.

Ushindi mkubwa mfano wa mabao 3-0 utampa kazi mpinzani kwenda kushinda mabao 4-0 ugenini, lakini ukiruhusu moja ikawa 3-1, anakuwa na kazi ya kusaka mabao 2-0 tu ili asonge mbele. Lakini ushindi kama wa mabao 4-0 utamfanya mpinzani afikirie namna ya kushinda 5-0 nyumbani kwake, hivyo uzembe na mbwembwe za kutaka kupiga chenga langoni, mpira ukaporwa na kuwekwa wavuni matokeo yakawa 4-1, yanamrahisishia kazi nyumbani.

Sisi tunaamini katika soka lolote linawezekana hasa kutokana na uzoefu na ubora wa Simba na Yanga, zinaweza kushinda kwa idadi ndogo ya mabao na kwenda kutoa sare au kushinda ugenini, lakini hali hii inaleta presha kubwa kwa wachezaji, benchi la ufundi, viongozi na hata mashabiki, hivyo ili kuondoa hilo na kuwafanya wachezaji kwenda ugenini wakijiamini na kuwapa presha kubwa wapinzani, ni kushinda idadi kubwa ya mabao, tena bila kuruhusu bao nyumbani.

Tunaamini muda wa kufanya maandalizi ya mwisho na kuwajenga wachezaji kisaikolojia bado upo, lakini pia tunawataka mashabiki kuendelee kununua tiketi kwa wingi ili kujaza uwanja siku hiyo mechi kutimiza vema nafasi ya mchezaji wa 12 uwanjani kwa kuzisapoti timu zao mwanzo mwisho.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Adam Fungamwango

# Waamuzi kutoka nje wataleta utulivu wa mashabiki Ligi Kuu

**MIAKA** ya nyuma baada ya waamuzi wa Tanzania kuonekana kudorora kwenye uchezeshaji na kufanya makosa mengi, baadhi ya wadau walipendekeza waletwe marefa kutoka nje kwa baadhi ya mechi.

Wadau walipendekeza waamuzi kutoka nje ya Tanzania wawe wanaletwa kuchezesha mechi kubwa, zenye maamuzi, utata na hata michezo ya 'dabi.'

Mfano mechi za Simba na Yanga, na Azam dhidi ya timu hizi mbili ni moja kati ya mechi zilizokuwa zikipendekezwa kuchezeshwa na waamuzi hao.

Hata hivyo, Chama cha Waamuzi Tanzania na hata kamati yao, ilikuwa ikipinga na kusema bado waamuzi wazawa wana uwezo wa kuchezesha mechi za Ligi Kuu bila matatizo.

Pamoja na kutolewa mifano mingi ya 'dabi' zilizochezeshwa na waamuzi kutoka nje hapa hapa Afrika, kwenye nchi za Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, Afrika Kusini, Misri, Morocco, Tunisia, lakini bado walionekana kupinga.

Hakuna aliyesema kuwa waamuzi wa Tanzania hawawezi kuchezesha, ila wakati mwingine ni kuwapunguzia mzigo wa lawama tu kwani mechi ikichezeshwa na waamuzi kutoka nje, hata kama kutakuwa na makosa ya kibinadamu mashabiki wataamini hivyo, tofauti na ikitokea kwa refa mzawa.

Anaweza kuambiwa amechukua mlungula au mashabiki wakasema wanamfahamu anakaa maeneo fulani, ni shabiki wa timu fulani tangu zamani.

Hizo ni changamoto wanazozipata waamuzi wa hapa nchini, lakini pia mabosi wa soka kwenye nchi nilizozitaja hapo juu hawakuwa wajinga kuruhusu waamuzi kutoka nje kuchezesha baadhi ya michezo migumu na inayovuta hisia za mashabiki wengi, ila ni kuepuka mambo kama hayo.

Wadau walipozidi kujenga hoja lilikuja suala la kutokuwa na kanuni ambayo itawawezesha si wachezaji kutoka nje ya nchi tu kuchezesha Ligi Kuu Bara, bali hata kutoka Zanzibar.

Hatimaye baada ya kipindi kirefu, milango imefunguliwa kwani msimu ujao waamuzi kutoka Sudan wataruhusiwa kuchezesha Ligi Kuu Tanzania Bara.

Kwanza kabisa Rais wa Shirikisho la Mpira wa Miguu (TFF), Wallace Karia, ameshatangaza kuwa kutakuwa na Teknolojia ya Kusaidia Waamuzi (VAR) mbili, moja ikifungwa Uwanja wa Benjamin Mkapa na nyingine inayotembea, 'Mobile VAR.'

Hii ya pili akasema itatumika kwenye viwanja vya mikoani, lakini akaainisha, Simba na Yanga zitapewa kipaumbele kwa sababu michezo yao ndiyo inayofuatiliwa zaidi na ndiyo yenye malalamiko mengi.

Kingine ni ujio wa klabu ya Ligi Kuu ya Sudan, Al Hilal, pamoja na waamuzi wao. Bosi wa Waamuzi, Nassor Hamdoun, akaunga mkono.

"Tukumbuke mahusiano kutoka nje ni moja ya jambo bora katika kuwaendeleza waamuzi wetu, kumekuwa na taarifa ambazo zimeshatolewa ufafanuzi na TFF kwamba kuna waamuzi kutoka nje ya nchi wapo hapa na wenyewe watajumuishwa kwenye ligi yetu, nawahakikishia wadau na wao wenyewe kuwa tutakuwa nao sambamba na ninawaomba waamuzi wenzangu wasione kama vile wanaingiliwa, hapana. "Hii ni changamoto, ni lazima wakubaliane nayo, tushirikiane nao kwa namna ya kuwaongezea wao kitu na sisi pia kupata kitu kutoka kwao, wote tujifunze, tunaunga mkono hilo," alisema bosi huyo wa waamuzi nchini.

Binafsi, naunga mkono waamuzi kutoka nje ya nchi kuchezesha Ligi Kuu ya Tanzania kwa sababu ni jambo lililopigiwa sana kelele huko nyuma, ukichanganya na kuwapo kwa VAR, nadhani nchi itakuwa na ligi bora yenye maamuzi sahihi zaidi ambayo itavutia mashabiki, wadhamini na wawekezaji wengi.

Kama itakavyokuwa VAR kwa jinsi alivyoshauri Karia, na mimi nashauri waamuzi hawa wa nje, wapewe kuchezesha mechi zile tu ambazo zinakamata hisia za mashabiki wa soka nchini ili kuleta utulivu kwa mashabiki kwa sababu wanachezeshwa na mgeni.

Naamini uwapo wa waamuzi hawa utaongeza kitu ambacho mashabiki hawajawahi kukiona kiasi kwamba hata machafuko kwenye nchi yao yakimalizika na kuamua kurudi nchini mwao kuna vitu tutakuwa tumejifunza na nadhani hata TFF na kamati wataamua kusaka tena waamuzi kutoka nchi nyingine kwa ajili ya kuwapiga 'kampani' marefa wa Tanzania.




Katibu Mkuu wa CCM Taifa, Balozi Emmanuel Nchimbi, akihutubia Mabaraza ya Wazee wa CCM Mkoa wa Kusini na Kaskazini Pemba, Makonyo Wilaya ya Chake Chake.
**PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Nchimbi athamini mchango wa wazee kuleta maendeleo

**NA Is-Haka Omar,** PEMBA

KATIBU Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Taifa, Balozi Dk. Emmanuel Nchimbi, amesema maendeleo yaliyofikiwa nchini yametokana na juhudi za kiutendaji zilizoasisiwa na wazee wa chama hicho waliohudumu kwa bidii na maarifa katika sekta za umma na binafsi.

Alisema hayo katika ziara yake siku moja wakati akizungumza na kujitambulisha kwa Mabaraza ya Wazee wa CCM wa mikoa ya Kaskazini na Kusini Pemba.

Balozi Nchimbi alisema CCM inaendelea kuimarika kisiasa, kijamii na kiuchumi kutokana na misingi mizuri iliyowekwa na wazee wa chama hicho enzi za utumishi wao toka walipoviunganisha vyama vya ASP na TANU na kuzaliwa kwa CCM mwaka 1977. Alisema wazee hao wamefanya kazi kubwa ya kuasisi Mapinduzi ya Zanzibar na Muungano wa mwaka 1964 kwa dhamira za kuikomboa nchi kutoka katika mikono ya kisultani na kikoloni.

Dk. Nchimbi, alisema inatambua mchango mkubwa wa wazee wa chama hicho kwa juhudi zao za kuitumikia nchi kwa uadilifu na ndio kielelezo cha kifikia maendeleo endelevu nchini.

Kadhalika, lengo la ziara hiyo ni kukutana na wazee hao ili kubadilishana nao mawazo na kusikiliza changamoto, ushauri na mapendekezo yao ya kuimarisha masuala mbalimbali ya kisiasa ndani ya CCM.

"Tunathamini juhudi zenu kwani enzi zenu mlitumikia nchi kwa juhudi kubwa mkaanzisha Chama Cha Mapinduzi na kuweka misingi imara inayotuongoza hadi hivi sasa hivyo nakuombeni muendelee kutushauri na kutuelekeza pale mtakapoona tunaenda kinyume na misingi hiyo," alisema Dk. Nchimbi.

Pia, alikemea vitendo vya ubaguzi wa kiitikadi, kidini na kikabila na kuonya kama vitendo hivyo visipokemewa vinaweza kuingiza nchi katika machafuko ya kisiasa.

Alipongeza hatua kubwa ya mafanikio iliyofikiwa na serikali ya awamu na nane chini ya Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Hussein Mwinyi katika nyanja za kisiasa, kiuchumi na kijamii.

Aliwasihi wanachama wa CCM na wananchi kwa ujumla kuendelea kumuunga mkono Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Samia Suluhu Hassan ili afikie maono ya kuongoza nchi kwa ufanisi zaidi.

Naye Naibu Katibu Mkuu wa CCM Zanzibar Dk. Mohamed Said Dimwa, alisema kupitia kitabu cha taratibu za sehemu ya wazee wa CCM toleo la 2019 ibara ya 10(2) inafafanua kuwa wazee ni hazina kubwa ya busara, hekima, uzoefu wa kuendesha shughuli za chama na maendeleo ya nchi.

Dk. Dimwa, alisema CCM Zanzibar ipo imara na itaendelea kutekeleza siasa za kistaarabu zinazozingatia ushindani wa sera kwa vitendo huku ikijipanga kuhakikisha inashinda kwa kishindo katika uchaguzi mkuu ujao wa mwaka 2025. Katibu wa Wazee wa CCM Mkoa wa Kusini Pemba, Hanuna Ibrahim Masoud, alisema wamefurahishwa na uteuzi wa Dk. Nchimbi kwa kuwa ni kiongozi mchapakazi, mbunifu, mzalendo na anayekijua vizuri Chama cha Mapinduzi na jumuiya zake.

# MOI yapokea wagonjwa wanne wa kiharusi kila wiki

**Na Joseph Mwendapole**

TAASISI ya Mifupa na Ubongo Muhimbili (MOI), imesema inapokea wastani wa wagonjwa wanne wa kiharusi kila wiki wengi wao wakiwa vijana wa miaka 30 hadi miaka 50.

Hayo yalisemwa mwishoni mwa wiki na daktari bingwa wa upasuaji wa ubongo, mgongo na mishipa ya fahamu MOI, Dk. Alpha Kinghomela ambaye ni mratibu wa mafunzo ya kiharusi.

Alikuwa akizungumzia mafunzo ya tiba bobezi ya teknolojia ya hali ya juu inayotumika duniani kwasasa ya kutibu wagonjwa wa kiharusi.

Teknolojia hiyo inahusisha kufanya upasuaji wa ubongo kwa kutumia mishipa damu ya kwenye paja na mafunzo hayo yametolewa na Prof. Cagin Senturk kutoka Uturuki.

Alisema mafunzo hayo yalijumuisha washiriki kutoka Hospitali ya Taifa Muhimbili na Mloganzila.

"Wengi wa wagonjwa tunaopokea ni vijana umri kuanzia miaka 30 hadi 50, kiharusi ni tatizo namba moja duniani kwa kusababisha ulemavu wa kudumu wa viungo na la pili kwa kusababisha vifo," alisema.

"MOI tumejipanga kuwa kituo cha umahiri cha Tiba ya Kiharusi (Stroke) barani Afrika ikiwa ni utekelezaji wa maelekezo ya serikali ya kuanzisha vitengo vya tiba ya kiharusi," alisema.

Alitaja sababu kubwa za ugonjwa wa kiharusi ni pamoja na shinikizo la damu, magonjwa ya moyo, kisukari na maumivu makali ya kichwa na kushauri kuwa ni vyema mtu mwenye dalili hizo akawahi hospitali kwa ajili ya uchunguzi wa awali ili kudhibiti madhara yasitokee.

Mwezeshaji wa mafunzo hayo, Prof. Senturk alisema hayo ni mafunzo ya kwanza ya kutibu kiharusi kutolewa katika ukanda wa Afrika ya Mashariki na Kati na yataiwezesha MOI kuwa kituo mahiri na cha rufaa cha wagonjwa wenye matatizo hayo katika ukanda wa Afrika Mashariki.

"Mafunzo haya ni ya kwanza kutolewa Afrika Msharikí na Kati na nimeona MOI imejiandaa vyema kwa kuwa na vifaa vya kisasa vya kutolea tiba ya kiharusi, ni imani yangu kuwa MOI itakuwa kituo cha umahiri cha tiba na rufaa ya Kiharusi katika ukanda huu," alisema Prof. Senturk.

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA YA TANZANIA

Katika mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya MWANGA
Kituo cha MWANGA Mkoa KILIMANJARO

Usimamizi wa mirathi Na. 03/2024

KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA
MAREHEMU HABIBU SALEHE ABDALLAH WA MWANGA
KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI
YALIYOLETWA
NA SAIDI MUHAMEDI NGULUMA

**TANGAZO**
**(kanuni ya 5(2) ya kanuni za Usimamizi wa Mirathi Makama za Mwanzo)**
Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 04 mwezi 04 mwaka 2024 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
**Zingatia;**
Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
Imetolewa leo tarehe 01 Mwezi 03 Mwaka 20254

HAKIMU
HAKIMU MKAZI
MAHAKAMA YA MWANZO
MWANGA

KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**MARIANUS EVARISTO KOMBA** anatangaza kupotea kwa kadi ya pikipiki yenye usajili namba **MC 381 CPR.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
POLISI TAARIFA:
**9910840438933**

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA YA TANZANIA

Katika Mahakama ya Mwanzo ya CHAMWINO MJINI
Wilaya ya DODOMA

Kituo cha CHAMWINO MJINI Mkoa DODOMA

Shauri la Madai Na. 55/2024

JINA LA MDAI ........... MAGUCHI MICROFINANCE CO. LTD

JINA LA MDAIWA .................... BAKARI SEIF NALINGA

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(Kanuni ya 18 ya kanuni za taratibu Madai katika Mahakama za Mwanzo)**

KWA
BAKARI SEIF NALINGA
MIYUJI- DODOMA

**Kwa kuwa mdai ameleta madai yake kwamba MADAI YA TSH. 6,500,000/=**

Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii tarehe 05 mwezi 04 mwaka 2024 saa 2:30 asubuhi kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima keleta shahidi/Mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.
**ANGALIZO:** Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini, Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila wewe kuwepo.
Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 22 Mwezi 03 Mwaka 2024

HAKIMU

KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**DAUDI ROMWADI NDUNGURU** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye usajili namba **T 468 AAX.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
POLISI TAARIFA:
**PHQ/RUV/SON/657/2024**

KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**EMILIO PAULO KALINGA** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **TOYOTA HIACE** yenye usajili namba **T 581 CVF.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
POLISI TAARIFA:
**PHQ/RUV/SON/851/2024**

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA YA TANZANIA

Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya DODOMA MJINI

Kituo cha CHAMWINO Mkoa DODOMA

Usimamizi wa mirathi Na. 11/2024

KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA
MAREHEMU MEDADI ANDREA NSOMEKE wa NKUHUNGU
KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI
YALIYOLETWA NA FLORA SILIVESTER MEDADI

**TANGAZO**
**(Kanuniya 5(2) ya Kanuniza Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya Marehemu tajwa hapo juu,wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 04 Mwezi 04 Mwaka 2024 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
Zingatia;
Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
Imetolewa leo Tarehe 19 Mwezi 03 Mwaka 2024.

KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**LEO MAPUNDA** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye usajili namba **T 197 BLL.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
POLISI TAARIFA:
**SO/RB/3323/2021**

# Prof. Wangwe: Uchumi wa nchi unakua, wananchi bado maskini

**Na Enock Charles**

MTAALAMU wa Uchumi, Prof. Samuel Wangwe amesema uchumi wa Tanzania unakua, lakini bado kuna umaskini mkubwa kwa wananchi.

Prof. Wangwe alitoa kauli hiyo mwishoni mwa wiki katika Chuo Kikuu cha Dar s Salaam (UDSM) wakati wa uzinduzi wa 'Deep Challenge Fund', mfuko utakaotoa fedha za ruzuku kwa watafiti ili kufanya utafiti wa hali ya umasikini nchini.

Utafiti huo unalenga kupata mbinu sahihi za kupambana na umaskini huo ambao kasi ya kupungua kwake nchini imeonekana kuwa ndogo licha ya uchumi wa nchi kukua.

Prof. Wangwe aliwaambia waandishi wa habari, "pamoja na takwimu kuonesha uchumi wa nchi unakua, bado kuna umaskini mkubwa kwa wananchi, hivyo kuwapo haja kufanyika utafiti ili kuona sababu na kuzitafutia majibu. "Uchumi unakua lakini umaskini unapungua kidogo, ina maana kule kukua kuna watu wanapata faida ambao hata si maskini, tunakosea wapi?" alihoji Prof. Wangwe.

Alisema mfuko huo utawezesha kupatikana taarifa kutoka vyanzo vya chini kabisa; watafiti wakishuka chini, wataleta taarifa za uhakika ni kwa namna gani ukuaji uchumi unaweza kwenda sambamba na kupungua kwa umaskini.

Alisema uchumi ukikua, inatarajiwa umaskini nao utapungua, lakini kwa sasa viwanda haviongezi ajira inavyotakiwa; watu wanaondoka vijijini kuja mjini, ni kama wanakimbia umaskini, lakini wanakuja kukutana na umaskini mwingine.

Mkurugenzi Mkuu wa shirika hilo, ambaye pia ni Mwenyekiti Mwenza wa Kamati ya Uongozi ya Taifa ya Deep Challenge, Dk. Charles Sokile, alisema watafiti wa Tanzania watashirikiana na watafiti wengine duniani kupata takwimu ambazo zinaweza kutumiwa na serikali katika kupambana na umaskini ambapo alisema kila andiko la mradi wa utafiti linaweza kupatiwa Pauni 5,000 (Sh. milioni 15) hadi Pauni 50,000 (Sh. milioni 150) kwa utafiti utakaofanyika kati ya miezi sita hadi 12.

Mtafiti kutoka Shule Kuu ya Biashara UDSM (UDBS), Winnie Muangi, alisema ufadhili huo utasaidia watafiti wengi wa Kitanzania kupata uwezo wa kufanya utafiti katika maeneo mbalimbali utakaosaidia serikali na watunga sera katika mikakati ya kupambana na umaskini nchini.

"Sisi (watafiti) tunaona kabisa bado kuna pengo katika utekelezaji sera na mipango mbalimbali iliyopo, utafiti utasaidia kutoa taarifa jinsi gani pengo hilo linaweza kutatuliwa kwa ajili ya kusaidia maendeleo katika taifa," alisema Winnie.

Mnamo Juni 1999, Tanzania ilianza kutekeleza Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, ambayo ina dhima kuu ya kupunguza walau nusu ya watu wanaoishi katika umasikini na kuwafanya waishi katika uchumi wa kati kufikia mwaka 2025.



Mkaguzi Msaidizi wa Jeshi la Polisi Kitengo cha Dawati la Jinsia na Watoto wilaya ya Kawe, Frank Mnojela akitoa elimu ya kupinga vitendo vya ukatili wa kijinsia kwa madereva wa pikipiki katika kituo cha Africana jijini Dar es Salaam ukiwa ni mwendelezo wa maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani kwa udhamini wa kampuni ya Barrick jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# 'Kupika kwa kuni ni sawa na kuvuta sigara 300 kwa siku'

**Na Gwamaka Alipipi**

MBUNGE wa Ilala, Mussa Zungu ametangazia neema mamalishe na babalishe katika Soko la Samaki la Kimataifa Feri, akisema watafungiwa mtungi mkubwa wa nishati safi ya kupikia ili kuwaepusha na hatari ya mlipuko wa moto na gharama ya kununua gesi.

Vilevile, ameonya kuwa kupika kwa kutumia kuni au mkaa kuna madhara kiafya kwa kuwa ni sawa na kuvuta sigara 300 kwa siku.

Zungu alitoa ahadi hiyo mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam wakati akigawa mitungi 200 kati ya 700 iliyotolewa kwa mamalishe na babalishe na kampuni ya gesi ya ORYX Tanzania.

Pamoja na mambo mengine, Zungu aliwataka Watanzania kubadilika na kumuunga mkono Rais Samia Suluhu Hassan katika kampeni ya kutumia nishati safi ya kupikia ili ifikapo mwaka 2030, asilimia 80 ya Watanzania wawe wanatumia nishati hiyo.

Alisema kutumia kuni na mkaa kwa sasa ni sawa na mtu mmoja kuvuta sigara 300 kwa siku, kwamba madhara yake yatakuja kuonekana baadaye na ndiyo maana Rais Samia ameanzisha kampeni ya nishati safi ya kupika ili Watanzania waishi maisha marefu na salama kiafya.

"Mkombozi wetu ni Rais Samia ambaye alianzisha kampeni ya nishati safi ya kupikia, kuhakikisha Watanzania wanaishi maisha mazuri. Kwahiyo, tukubali kubadilika na kutumia nishati safi ya kupikia kwa ajili ya kutunza afya zetu na mazingira," alisema Zungu. Kuhusu ahadi ya kufunga mtungi wa gesi katika soko hilo, Zungu ambaye pia ni Naibu Spika wa Bunge, alisema kilio hicho ni cha muda mrefu, hivyo ameshazungumza na kampuni ya ORYX ambayo imekubali kufunga mtungi huo wa kisasa utakaosambaza huduma hiyo kwa wafanyabiashara takribani 200 kwa bei nafuu.

Awali akiwasilisha kilio cha wafanyabiashatra hao, kiongozi wa zoni namba saba katika soko hilo, Said Mpinji, aliomba serikali iwafungie mtungi mmoja mamalishe na babalishe wa soko hilo kwa kuwa sasa kuna mitungi mingi midogo inayotumika, hali inayohatarisha usalama.

Mkurugenzi wa kampuni ya gesi ya ORYX Tanzania, Benoit Araman alisema wamepokea ombi la Naibu Spika la kufunga tangi la gesi katika soko hilo.

"ORYX Gas tunaamini kwamba ukipika kwa kutumia gesi inaleta maendeleo mengi kwa jamii yetu pia inalinda mazingira kwa kuacha kukata miti.

"Zaidi ya yote ni kulinda afya ya wanawake kwa kuwaepusha kuvuta moshi na mvuke unaoathiri mapafu na afya yao unaotokana na kuni na mkaa," alisema.

Alisema ORYX inatekeleza agizo la serikali kwa kuhakikisha taasisi zenye watu zaidi ya 100 wanatumia nishati safi kwa kutengeneza mifumo salama ya gesi kwa kutumia tangi kubwa, kwamba mifumo hiyo inaweza kutumika shuleni, kambi za jeshi, vyuo vya polisi na magereza.

Alisema hadi sasa kampuni hiyo imeshatoa mitungi ya gesi pamoja na majiko zaidi ya 10,000 katika taasisi mbalimbali na wajasiriamali.

Meneja wa soko hilo, Selemani Mfinanga, alisema wajasiriamali katika soko hilo wanakabiliwa na matatizo mbalimbali, ikiwa ni pamoja na ubovu wa miundombinu ya kuunganisha gesi na mifumo ya gesi kutoboreshwa, hali inayosababisha kutumia gharama kubwa.

# Mgodi waikosha Kamati ya Bunge utunzaji mazingira

**Na Joctan Ngelly,** GEITA

KAMATI ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC) imepongeza mgodi wa dhahabu Bukcreef kwa kuhifadhi na kutunza mazingira.

Makamu Mwenyekiti wa kamati hiyo, Japhet Hasunga, alitoa pongezi hizo mwishoni mwa wiki walipozuru mgodini huko katika Kijiji cha Lwamgasa, mkaoni Geita.

Alisema wamefurahishwa kuona mgodi unashiriki kutunza mzingira ambayo ni uhai wa nchi; wakitunza uoto wa asili na kutekeleza kampeni ya kupanda miti.

"Lengo la Kamati yetu kuja hapa kwenye mgodi wa Buckreef ni kuona namna fedha za umma zinavyotumika, zile ambazo zinapitishwa na Bunge, kila mwaka Bunge limekuwa linapitisha bajeti na likielekeza hizo fedha kwenda taasisi mbalimbali kwa ajili ya kutekeleza majukumu.

"Sasa leo tumekuja kuangalia fedha ambazo walipewa STAMICO, zimefanya kazi ilikusudiwa na Bunge? Hicho ndicho kitu ambacho tumekuja kukiangalia, pia tumekuja kuangalia thamani hasa ya hizo fedha, zimeleta nini kwenye taifa hili?" Hasunga alisema.

Alisema wamefurahi kuona Buckreef inatoa ajira kwa watanzania, akibainisha kuwa aslimia 100 ya wafanyakazi wa mgodi wa Buckreef ni Watanzania.

Hasunga alisema changamoto ya umeme wameiona, akiitaja mashine ya pili inayotegemea kuwashwa mwishoni mwa mwezi huu kwenye Bwawa la Nyerere, itapunguzwa tatizo la umeme wa ratiba.

Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya STAMICO, Venance Mwasse, alisema changamoto zinazojitokeza katika mgodi wa Buckreef ni umeme huo wa ratiba na wananchi kuvamia kwenye leseni ya mgodi huo.



# Balozi ataja mbinu kukuza lugha asili

**Na Halfani Chusi**

BALOZI wa Uswisi nchini Tanzania Didier Chassot, amesema ili kukuza na kuonesha tofauti ya tamaduni katika mabara ya Afrika, America na Ulaya yanapaswa kuenzi na kukuza lugha za asili.

Aliyasema hayo mwishoni mwa wiki katika hafla ya kusherehekea siku ya nchi zinazozungumza lugha ya Kifaransa duniani iliyofanyika nyumbani kwake, jijini Dar es Salaam.

Alisema watu zaidi ya milioni 321 wanazungumza Kifaransa duniani hali inayofanya kuwa lugha ya tano inayozungumzwa na watu wengi na pekee kwenye mabara matano.

"Ni muhimu kuzingatia kwamba karibu asilimia 60 ya wanaozungumza Kifaransa wapo katika Bara la Afrika kufikia mwaka 2060 zaidi ya watu milioni 700 watakuwa wanaishi katika nchi zinazozungumza Kifaransa na asilimia 75 watatoka katika bara la Afrika," alisema Balozi Chassot.

Alisema kwao ni furaha kusherehekea siku hiyo kwa kuwa nchini kwao, lugha ya Kifaransa inatumika na robo ya wakazi wake.

Katibu Mkuu Wizara ya Sanaa na Michezo, Gerson Msigwa, aliusifu ubalozi huo kusherehekea siku ya lugha yao mama akiahidi Tanzania itatumia mbinu hiyo kukuza Kiswahili.

Alisema Tanzania ipo katika kampeni ya kukikuza Kiswahili, na takwimu zinaonyesha kuna wazungumzaji milioni 500 ndani na nje nchi.

"Tunakokwenda lugha ya Kiswahili kasi yake ni kubwa, inapendwa duniani na inatusaidia kudumisha mila na desturi zetu, kuzalisha ajira, kuvutia uwekezaji, na mpaka sasa tayari imekuwa lugha rasmi kwanye Jumuiya ya Umoja wa Afrika, Afrika Mashariki na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) dalili hizi ni njema kwa ukuaji wake," alisema Msigwa.



Meneja Uchunguzi wa Kampuni ya Teknolojia na Mawasiliano, Vodacom Tanzania, Joseph Mnyune akitoa elimu kwa mawakala wa kampuni hiyo ili kuwaongezea ujuzi wa kutambua, kudhibiti na kuelimisha wateja juu ya ulaghai na utapeli kupitia simu za mkononi jijini Arusha mwishoni mwa wiki. Pembeni yake ni Meneja Mauzo Mwandamizi wa Vodacom Tanzania kanda ya Kaskazini, Andrew Temu.**PICHA:MPIGAPICHA WETU.**

# Mil.291/- kupeleka maji Kijiji cha Gadabagara

**Na Jaliwason Jasson,** MANYARA

KERO ya maji iliyokuwa ikiwalazimu wanawake na watoto wa Kijiji cha Gadabagara, Wilaya ya Babati, mkoani Manyara, kupoteza zaidi ya saa nne hadi tano kila siku kusaka maji kwenye madimbwi, hatimaye imepatiwa ufumbuzi.

Zaidi ya kaya 360 zenye wakazi 1,509 katika kijiji hicho, sasa zimeanza kunufaika na maji ya bomba, baada ya Shirika la World Vision Tanzania (WVT), kutekeleza mradi wenye thamni ya zaidi ya Sh. milioni 291.669.

Meneja wa World Vision (WVT), Kanda ya Kaskazini, Juliana Charles, alisema gharama za ujenzi umeigharimu kiasi cha Sh. milioni 291.669 hadi kukamilika kwake.

Juliana, alieleza hayo wakati wa hafla ya kukabidhi mradi huo, uliotekelezwa na WVT kwa kushirikiana na Wakala wa Maji Vijijini, Wilaya ya Babati (RUWASA).

"Ili kuufanya mradi huu kuwa endelevu na kuwanufaisha vizazi kwa vizazi, tumeanza kutoa mafunzo kwa kamati ya maji ya kijiji, juu ya namna ya usimamizi na uendeshaji wa mradi huu," alisema Charles.

Aidha, alisema maji yaliyochimbwa yalipimwa na kuthibitishwa kuwa ni safi na salama na yanakubalika kwa matumizi ya binadamu.

Kwa mujibu wa meneja huyo, mradi huo unawanufaisha pia wanafunzi wa Shule ya Msingi Gidabagara, yenye watoto 610 baada ya kupata maji ya bomba.

Mkurugenzi wa World Vision Tanzania, Simon Moikani, alisema wao wanahitaji kuona miradi waliyoanzisha inakuwa endelevu baada ya kukamilika.

"RUWASA mnaweza mkatuma wataalamu Lake Eyasi (Ziwa Eyasi), ili wajifunze namna ya kutunza miradi ikawa endelevu, na mkawa mnakusanya fedha nyingi," alisema Mkurugenzi huyo.

Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Queen Sendiga, alionyesha kuridhishwa na ujenzi wa mradi huo, unaozalisha lita za ujazo za maji 50,000 kwa siku.

Sendiga, alisema licha ya vitongoji vitatu kuanza kupata maji kupitia mradi huo, aliagiza RUWASA kuvipelekea maji vitongoji viwili vilivyobakia.

Pia, alisema vilula 10 vya kutoa huduma ya majisafi na salama vilivyopo katika kijiji hicho havitoshi, huku akiagiza RUWASA kuongezea vingine.

"Suala la upatikanaji wa maji, siyo la kubahatisha ni la kimkakati. Na wananchi kupata maji hawajafanyiwa hisani, ni haki yao ya msingi,"alisema.

Mmoja wa wakazi wa Kijiji cha Gidabagara, Halima Shaban, alisema kabla ya kutekelezwa kwa mradi huo, walikuwa wakitumia maji ya madimbwi yaliyowasababishia maradhi, ikiwamo magonjwa ya mlipuko.

# Serikali yaanzisha kampeni kurudisha uoto wa asili Same

**Na Ashton Balaigwa,** SAME

SERIKALI imeanzisha kampeni maalumu iitwayo 'Tuifanye Same kuwa kijani', ambapo pamoja na mambo mengine, miti ya aina mbalimbali ikiwemo ya matunda na vivuli itapandwa ili kuhimili mabadiliko ya tabianchi na kurejesha uoto wake wa asili.

Uamuzi wa kuanzisha kampeni hiyo, unatokana na Wilaya ya Same iliyoko mkoani Kilimanjaro, kwa kipindi kirefu kuathiri uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara.

Akizungumzia kampeni hiyo, Mkuu wa Wilaya ya Same, Kasilda Mgeni, alisema kampeni hiyo iliyoanza Novemba mwaka jana, tayari kumeshapandwa miti 512,000.

"Kupitia kampeni hii ya Ifanye Same kuwa ya kijani, tumepanda miti katika barabara kuu na yote imestawi kwa kuwa tulipanda kipindi cha mvua zikinyesha," alisema Mgeni.

Mkuu huyo wa wilaya hiyo, alisema mbali na kampeni hiyo, lipo agizo la kila halmashauri kupanda miti milioni moja, nalo limeshatekelezwa ambapo mpaka sasa wamefanikiwa kupanda miti milioni 1.7 katika kipindi cha mwaka 2023/24.

Alisema Same inatikiswa na mabadiliko ya tabianchi kwa muda mrefu, hivyo kama wilaya wameona njia pekee ni kurudisha uoto wa asili kwa kupanda miti katika maeneo mbalimbali, ikiwemo ya taasisi za serikali na zisizo za kiserikali.

"Haya mabadiliko yaliyoikumba Same kwa kiasi kikubwa yamesababishwa na uharibifu wa mazingira ikiwemo ukataji wa miti na kuchangia kuwepo kwa mafuriko yasiyo ya kawaida" alisema Kasilda.

Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Nurdin Babu, alisema Wilaya ya Same ipo zaidi barabarani, hivyo inapaswa kupanda miti ya kutosha katika maeneo hayo ili kuifanya kuwa ya kijani.

Babu alimwagiza mkuu huyo wa Wilaya ya Same, kuhakikisha anachukua hatua kali kwa wote wanaofanya uharibifu wa miti inayopandwa katika wilaya hiyo, ikiwemo wafugaji ambao wamekuwa wakingiza mifugo yao nyakati za usiku kwa ajili ya malisho.

Alisema: "Hatuwezi sisi kupanda miti kwa ajili ya kupambana na uharibifu wa mazingira halafu wafugaji wanavizia usiku viongozi wamelala wanaingiza kulishia mifugo yao na kufanya uharibifu kwenye miti yetu, Mkuu wa Wilaya chukua hatua kali atakayebainika ikiwemo kuitafisha hiyo mifugo".





# Viongozi kituo cha mabasi wadaiwa kutafuna mabilioni

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WALIOKUWA viongozi wa Umoja wa Mawakala na Wajasiriamali katika Kituo cha Mabasi Kahama (CDT) wanadaiwa kufuja fedha za umoja huo Sh.milioni 19.872.

Hoja ya ubadhirifu huo iliibuliwa juzi na Mwenyekiti wa Wajasiriamali, Shukuru Peter wakati wa hafla na Mkuu wa Wilaya hiyo, Mboni Mhita.

Alisema kiasi hicho cha fedha kinadaiwa kuliwa na waliokuwa viongozi wa CDT na zinatokana na vyanzo mbalimbali vya mapato ikiwemo ada ya uanachama, ulinzi na faini za kikundi.

Alitaja viongozi hao kuwa ni aliyekuwa mwenyekiti, Sylvester Opata, Katibu, Baraka Simon na Yohana Ntambi, Ester Onesmo, Chande Ramadhani, Shabani Ndenje ambao wote walikuwa watia saini wakati wa kwenda kuchukua fedha benki.

Aidha aliomba serikali kuingilia kati suala ambalo alisema limesababisa migogoro ya mara kwa mara pamoja na mpasuko katika umoja huo.

Diwani wa Kata ya Kahama Mjini, Hamidu Kapama alikiri kuwepo kwa migogoro hiyo ya mara kwa mara juu ya fedha hizo zinazodaiwa kuliwa na wanapoomba kusomewa mapato na matumizi ya namna zilivyotumika hawakupewa majibu.

Kaimu Mkurugenzi wa Manispaa ya Kahama, Robert Kwela alisema awali umoja huo ulikuwa vizuri hali iliyowafanya kukopeshwa zaidi ya Sh.milioni 100 kwa lengo la kukuza mitaji yao, lakini kwa sasa umerudi nyumba kutokana na migogoro hiyo.

Kutokana na hali hiyo, Mboni alitoa muda wa siku saba kwa Jeshi la Polisi kuhakikisha linawatafuta viongozi hao ili watoe majibu ya fedha hizo zilipo au kuzirejesha na endapo watakaidi basi wachukulie hatua za kisheria.

# Mradi kuwawezesha wanawake katika kuongeza kipato kupitia uvuvi wazinduliwa

**Na Mwandishi Wetu**

MRADI wa kuwawezesha wanawake katika mnyororo wa thamani wa mazao ya uvuvi kwa nchi za Afrika Mashariki kupitia Ziwa Victoria umezinduliwa, utamwezesha mwanamke kuongeza kipato kupitia mazao hayo.

Akizungumza wakati wa kufunga mafunzo ya siku tatu ya Mtandao wa Wanawake Afrika Wanaojishughulisha na Uchakataji na Biashara ya Samaki (AWFISHNET), Mkurugenzi wa mradi huo, Suzanne Njeri alisema mradi huo utatekelezwa katika nchi za Tanzania, Kenya na Uganda.

Njeri alisema kuwa mradi huo wa majaribio utatekelezwa kwa kipindi cha miaka miwili na nusu na mpango ni kuwafikia wanawake 5,000 Afrika Mashariki, ambapo kwa kila nchi watakuwa wanawake 1,667.

Alisema mradi huo utakuwa na mambo mbalimbali ya kumuwezesha mwanamke lakini kubwa zaidi ni kumuinua kuanzia pale alipo ili aweze kuongeza uzalishaji wa mazao ya uvuvi.

Ofisa Uvuvi Mkuu kutoka Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Jovice Mkuchu alisema wizara imeweza kufanya tathmini mbalimbali kwenye sekta ya uvuvi, ambapo mradi unaenda kutatua changamoto za wanawake katika kupunguza upotevu wa mazao ya uvuvi tangu yanapovuliwa. Aidha, alisema wizara inashukuru uwepo wa mradi huo ambao umeona umuhimu wa kuwainua wanawake wa Tanzania katika Sekta ya uvuvi kwa kuwa wizara ni mlezi wa mtandao wa Wanawake Wanaojishughulisha na Uvuvi Tanzania (TAWFA) na kwamba wizara itakuwa bega kwa bega kuwezesha mradi huo kuwa na tija.

Mshauri Mkuu Elekezi wa mradi huo, Editrudith Lukanga alisema mradi unafadhiliwa na taasisi ya Bill and Melinda Gates kwa Dola za Marekani milioni 1.5 na utakuwa wezeshi kwa kuwa umewashirikisha wadau kuanzia ngazi ya chini.

Alisema katika utafiti waliofanya kwenye mialo mbalimbali wamebaini wanawake wamechukulia zao la samaki kama biashara, huku wakiwa na upungufu mkubwa wa wao wenyewe katika ulaji wa samaki na kukimbilia kuuza na kupata fedha ili wanunue chakula kingine au kununua mahitaji mengine ya familia.

Alisema kumekuwa pia na changamoto ya upatikanaji wa rasilimali fedha kama mtaji ili kuwasaidia wanawake kununua bidhaa kwa kiwango kikubwa ili kukidhi ushindani sokoni.

Pia, alitaja upotevu wa samaki kabla ya kuwafikisha sokoni baada ya kuvuliwa imekuwa ni changamoto kwa wanawake.

Mradi wa kuwawezesha wanawake katika mnyororo wa thamani wa mazao ya uvuvi Afrika Mashariki kwa sasa unatekelezwa kupitia Ziwa Victoria, lengo likiwa ni kufikia maeneo mengine ya Afrika ambayo yana maji ya asili ikiwemo bahari na maziwa.



Meneja wa Jiolojia wa Mgodi wa Dhahabu Buckreef Isaac Bunsansaba (kushoto) akimuonyesha mchanga wa dhahabu Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali ambaye pia ni Mbunge wa Vwawa Mkoani Songwe, Japhet Hasunga eneo la Kijiji cha Lwamgasa Mkoani Geita juzi. **PICHA: JOCTAN NGELLY**

# Wakazi walalamika kurukwa kupimiwa ardhi

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

WANANCHI wa Kijiji cha Bakima Manispaa ya Shinyanga, wamelalamika maeneo yao kurukwa wakati wa upimaji viwanja katika mradi wa urasimishaji makazi.

Walieleza kero hiyo juzi wakati wa ziara ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC), ilipotembelea utekelezaji wa mradi wa uboreshaji usalama wa miliki ardhi katika Kata ya Ibadakuli na Lubaga Manispaa ya Shinyanga.

Mmoja wa wananchi hao, Joseph Komanya, alisema kila wakati wamekuwa wakiambiwa wakae kwenye maeneo yao kwamba wanakuja kupimiwa ardhi, lakini wataalamu wamekuwa hawafiki.

Alisema hali hiyo ikawalazimu wahoji kwanini wao wanarukwa kupimiwa maeneo yao na kuambiwa eneo hilo lina mgogoro na Chama Cha Mapinduzi (CCM).

Alisema wanamiaka zaidi ya 30 wanaishi katika Kijiji hicho, lakini wanasikitika kurukwa kupimiwa maeneo yao, huku wakitajwa kuwa wavamizi wa eneo hilo.

"Haya maeneo tuliuziwa muda mrefu na tulipewa kabisa vikaratasi vya mauziano na viongozi, ambavyo kwa sasa hatuna kabisa vilishapotea sababu ilikuwa zamani sana, leo tunashagaa kuambiwa, hivyo tunaombeni msaada jamani," alisema Komanya. Ofisa Mipango Miji Manispaa ya Shinyanga, Emmanuel Mitinje alipotakiwa kujibu malalamiko hayo, alikiri ni kweli kijiji hicho wamekiruka katika upimaji kwa sababu kuna mgogoro huo na CCM.

Alisema kwa maelezo ya CCM wananchi hao awali walipewa eneo hilo waishi kwa muda, lakini wao wakajenga makazi ya kudumu na kung'ang'ania.

Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge PAC, Japhet Hasunga, aliiagiza Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, ikae na wananchi hao pamoja na CCM ili kuumaliza mgogoro huo.

Alisema sera ya Bunge inataka kila kipande cha ardhi kipimwe na kupangiwa matumizi kwa ajili ya kusonga mbele kimaendeleo.

Aidha, aliwataka pia wananchi wa Shinyanga wasiishie tu kwenye kupimiwa maeneo yao na kutambuliwa, bali wahakikishe washiriki zoezi hilo la urasimishaji makazi hadi hatua ya mwisho kwa kupata hati miliki ya maeneo yao. Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi Geoffrey Pinda, alisema mradi huo wa urasimishaji makazi umekuja kwa ajili ya utatuzi wa migogoro ya ardhi na mipaka.

Alisema atafanya ziara rasmi Shinyanga ili kutatua migogoro yote na kuwasaidia wananchi wamiliki maeneo yao kihalali.

# Nipashe Spotika



MECHI 5 ZA KUBURUDISHA LIGI YA MABINGWA ULAYA UK. 12-13




# WACHEZAJI WA5 ENGLAND WALIOCHEZA MECHI NYINGI

**LONDON,** England

DAIMA huonekana kama heshima ya juu zaidi kwa mchezaji wa mpira wa miguu kuvaa jezi nyeupe ya England.

Wachezaji huota ndoto ya kuweza kuiwakilisha nchi yao tangu mwanzo wa mchezo wao wa soka, huku wengine wakipigania maisha yao yote ili waonekane hata mechi moja kwa 'Simba Watatu' hao.

Hata hivyo, kuna nyota wengi ambao wamebahatika kuichezea England mara kwa mara kwa miaka mingi, na kuwa mastaa wa Wembley kwa uchezaji wao katika timu ya taifa.

Hawa ndio wachezaji watano wa England waliocheza mechi nyingi zaidi kwa kikosi cha England wa wakati wote.

### #5. Bobby Moore – Mechi 108

Mchezaji wa kipekee wa soka la England, Bobby Moore aliyewahi kuwa nahodha wa timu hiyo hadi kutwaa ubingwa wa Kombe la Dunia la 1966, akijiimarisha kama mmoja wa mabeki wa kati wakubwa zaidi kuwahi kutokea duniani.

Gwiji huyo wa West Ham United alikuwa mshindi wa pili katika tuzo ya Ballon d'Or ya 1970 na ni mmoja wa magwiji wa muda wote wa England.

Pamoja na Wright, beki huyo wa kati anajivunia rekodi ya pamoja ya kucheza mechi 90 kama nahodha wa England.

### #4. Steven Gerrard – Mechi 114

Gwiji huyu wa Liverpool pia alikuwa mtu mzuri sana kwa England kwa miaka mingi, Steven Gerrard, akiwa mmoja wa viungo wazuri waliovaa jezi nyeupe ya timu ya taifa.

Muda wake katika kikosi cha England haukuwa wa moja kwa moja kila mara, huku mijadala ikiendelea kuhusu iwapo yeye na Lampard wangeweza kucheza pamoja, lakini uwezo wake wa kucheza mechi kubwa na sifa zake za uongozi zilimfanya ajumuishwe kuwa muhimu kwa Simba Watatu.

Kwa kushangaza, yeye na Lampard wote walicheza mchezo wao wa mwisho kwa England dhidi ya Costa Rica kwenye Kombe la Dunia la 2014.

### #3. David Beckham - Mechi 115

Mmoja wa nyota wachache wa Kimataifa wa England kwa miaka mingi, David Beckham alijivunia kiasi cha kutisha cha kipaji chake asili. Ingawa alikuwa na wakati wake wa kutiliwa shaka katika kiwango cha kimataifa, jezi namba saba ilifanana na ustadi wake na 'uchawi' uwanjani.

Kiungo huyo alikuwa mmoja wa washambuliaji watamu wa soka ambao mashabiki wa England wamewahi kufurahia kuwashuhudia, na alikuwa mhusika maridadi ndani na nje ya uwanja.

Mechi 115 kwa England ni jumla ya kushangaza, na ni wachezaji wawili pekee wamesajili mechi nyingi zaidi yake.

### #2. Wayne Rooney - Mechi 120

Hadi Harry Kane anaingia uwanjani, Rooney alikuwa mfungaji bora wa England, akifunga mara 53 katika mechi 120. Mshambuliaji huyo wa Everton na Manchester United alitoa mfano wa mchezaji soka wa mtaani, na kuleta sifa hizo zisizo na kikomo kwenye uundaji wa timu ya taifa.

Atasikitika kwa kutokuwa na ushawishi zaidi kwenye michuano mikubwa, lakini Rooney bado anachukuliwa kuwa mmoja wa magwiji wa nchi hiyo katika karne ya 21.

Kazi ya kimataifa ya miaka 15 ilimalizika dhidi ya Marekani Novemba 2018.

### #1. Peter Shilton – Mechi 125

Peter Shilton aliweza kuichezea England mechi 125, huku mlinda mlango huyo akiwa na uwezekano wa kucheza zaidi katika miaka ya 1970.

Shilton alikuwa na nafasi ya kwanza katika miaka ya 1980 na alikuwa langoni la England wakati wa mchezo wa 'Bao la Mkono wa Mungu' dhidi ya Argentina kwenye Kombe la Dunia la mwaka 1986.

## ISIKUPITE

MSHAMBULIAJI wa Al-Nassr, Cristiano Ronaldo, ndiye mwanamichezo anayeingiza kiasi kikubwa zaidi cha fedha duniani kwa sasa, akiwa analipwa pauni milioni 175 kwa mwaka mbali na mshahara huo, pia anadhaminiwa na Nike, Tag Heuer, Armani na makampuni mengine ambapo kwa mwaka jana tu inakadiriwa aliingiza pauni milioni 218 kikiwa ni kiasi kikubwa zaidi kuliko mwanamichezo yeyote kuingiza.



## Extra Time



ARTETA



Wachezaji wa Arsenal wakishangilia baada ya kutinga robo fainali kwa kuitoa Porto ya Ureno kwa mikwaju ya penalti 4-2 kutokana na matokeo ya jumla kuwa 1-1. **PICHA: MTANDAO**

# MECHI 5 ZA KUBURUDISHA LIGI YA MABINGWA ULAYA

**LONDON,** England

ARSENAL itacheza na mabingwa wa Ujerumani Bayern Munich - wakiongozwa na nyota wa zamani wa Tottenham Hotspur, Harry Kane, huku mabingwa watetezi, Manchester City wakikabiliana na washindi walioivunja rekodi ya kulibeba kombe hilo, Real Madrid katika marudio ya nusu fainali ya mwaka 2022 na 2023.

**Je, Jude Bellingham wa Real atamshinda Rodri wa Man City? Je, Kylian Mbappe ataondoka Paris St-Germain na taji la Ulaya? Na je, 'Washikabunduki' wanaweza kuwa farasi weusi msimu huu?**

Hapa ndipo nafikiria mechi hizi zitakuwa na mpambano wa kushinda na kupoteza.

### Je, Arsenal watamzima Kane?

Furaha ya Arsenal ya kurejea katika robo fainali ya Ligi ya Mabingwa kwa mara ya kwanza baada ya miaka 14 huenda ilipunguzwa kidogo, wakati jina la mabingwa wa Bundesliga, Bayern Munich lilipotajwa.

Hii si kwa sababu hawawezi kumfunga Bayern Munich. Kwa kweli, huu ni mchuano ambao wanaweza kuishinda Bayern ambayo imekuwa na msimu mbaya nyumbani, ambapo wapo nyuma ya viongozi Bayer Leverkusen kwa pointi 10 kwenye msimamo wa Ligi Kuu Ujerumani na tayari wamefanya uamuzi wa kuachana na kocha Thomas Tuchel mwishoni mwa msimu.

Ni kwa sababu, kukiwa na moja ya mabadiliko hayo mazuri ya hatma ya Ligi ya Mabingwa Ulaya inaweza kuleta janga la zamani la Arsenal litarejea London Kaskazini katika umbo la nahodha wa England, Harry Kane, mfungaji bora wa muda wote kwa wapizani wao, Tottenham.

Kane aliondoka kwenda Ujerumani baada ya kufunga mabao 280 katika mechi 435 alizoichezea Spurs na hata wakati Bayern ikikabiliwa na matatizo mshambuliaji huyo amekuwa na kampeni nzuri, akiwa na hat-trick nne msimu huu katika ushindi wa 8-1 dhidi ya Mainz wiki iliyopita na kumfanya afikishe mabao 30 kati ya 25 katika mechi za ligi.

Arsenal wanaweza wasiwe na wasiwasi kuhusu Bayern, lakini watakuwa na wasiwasi kuhusu Kane. Na rekodi yake dhidi yao inaonesha kwa nini.

Kane alifunga mabao 14 katika mechi 19 dhidi ya Arsenal katika mashindano yote kwa kasi ya kufunga kila dakika 116. Alifunga 14 kati ya 17 kwenye Ligi Kuu England kwa bao moja kila dakika 107.

Arsenal, wakiwa na safu ngumu ya ulinzi ya Ligi Kuu msimu huu, watavutia kila mtu, lakini unaweza kuwa na uhakika Kane atakuwa ameongeza motisha dhidi ya adui huyo wa zamani, ambaye atakuwa na wasiwasi na athari yake ya kiwango cha kimataifa.

### Je, Bellingham atakuwa tofauti?

Jude Bellingham aliifungia Borussia Dortmund katika ushindi wa mabao 2-1 wa timu yake dhidi ya Manchester City katika msimu uliopita wa hatua ya makundi.

Manchester City na Real Madrid wamekuwa maadui wa mara kwa mara kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya baada ya kukutana katika nusu fainali kwenye misimu miwili iliyopita.

Real ilishinda mechi za mikondo yote miwili mwaka 2022, na kufunga mabao mawili dakika za lala salama kwenye Uwanja wa Santiago Bernabeu na kupeleka mchezo kwenye muda wa ziada, hatimaye kushinda na kisha kuifunga Liverpool kwenye fainali jijini Paris.

Msimu uliopita ulikuwa tofauti, ambapo Man City iliifunga Real mabao 4-0 kwenye Uwanja wa Etihad baada ya sare ya 1-1 nchini Hispania. Waliendelea kuifunga Inter Milan huko Istanbul na kutwaa taji hilo kwa mara ya kwanza kama sehemu ya mataji matatu pamoja na Ligi Kuu England na Kombe la FA.

Dakika 45 za kwanza za City katika mechi ya mkondo wa pili zitakumbukwa milele na wote walioshuhudia, huku hata mmiliki mpya wa Manchester United, Sir Jim Ratcliffe, akikiri hivi karibuni: "Zilikuwa bora zaidi ambao nimewahi kuziona."

Makocha wawili maarufu, Pep Guardiola na Carlo Ancelotti wanakutana tena - huku Real sasa wakijivunia mmoja wa vijana wenye vipaji vya hali ya juu kwenye mchezo ambaye watatumaini atageuza mkondo kwa niaba yao.

Nyota mpya wa Real, na soka la Ulaya, ni Muingereza Jude Bellingham. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 20, ameichukua Hispania kwa dhoruba na atakuwa mtu muhimu dhidi ya Man City.

Ancelotti atakumbuka masaibu ya msimu uliopita na atatumainii, pengine hata kutarajia, chipukizi huyo aliyesajiliwa kutoka Borussia Dortmund katika mkataba ambao unatajwa kuwa wa thamani ya pauni milioni 115 ataleta mabadiliko.

Real wana kundi la nyota, lakini macho ya wengi yataelekezwa kwa Bellingham katika robo fainali hii ya Ligi ya Mabingwa Ulaya maridadi na yenye hadhi ya juu zaidi. Ana tabia na uwezo wa kuamuru mchezo kwenye hatua ambayo ameonesha yuko nyumbani kabisa.

### Je, Walker atamnyamazisha Vinicius Jr?

Kyle Walker atakuwa na umri wa miaka 34 Mei, lakini beki huyo wa kulia wa Manchester City na England bado anaaminiwa na makocha wake wa klabu na nchi ili kuwadhibiti watu wenye majina makubwa kutokana na uzoefu wake na kasi yake ya kudumu.

Na ataombwa kufanya aina ya kazi kwa Mbrazil mahiri Vinicius Junior ambaye aliifanya katika ushindi wa kishindo wa City katika mechi mbili za nusu fainali msimu uliopita.

Wawili hao walijifunga katika mechi kali kwenye mkondo wa kwanza nchini Hispania, ambapo heshima iliisha hata kwa sare ya 1-1 na kwa kuoneshana heshima kubwa kati ya Walker na Vinicius Junior baada ya filimbi ya mwisho walipokumbatiana kwa furaha.

Vinicius Junior alikuwa ana bao la Real, lakini kasi na ufahamu wa Walker ulifanya mechi yao kuwa la kuvutia na itakuwa vivyo hivyo tena wakati huu.

Ni aina ya pambano binafsi ambalo Walker anafurahia, kama inavyothibitishwa pia na jinsi alivyotekeleza maagizo ya makocha, Gareth Southgate ya kumshinda Kylian Mbappe katika pambano lingine wakati Ufaransa ilipoichapa England 2-1 kwenye robo fainali ya Kombe la Dunia nchini Qatar 2022.

### Je, Arsenal watakuwa farasi weusi?

Arsenal ilifika nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa kwa mara ya mwisho mwaka 2009, ikiangukia kwa Manchester United.

Rekodi ya hivi karibuni ya Arsenal kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Bayern Munich si kitu cha kumfanya Kocha Mikel Arteta na wachezaji wake kuaminiwa.

Washikabunduki hao wamepoteza michezo yao mitatu iliyopita dhidi ya mabingwa hao mara sita wa Ulaya kwa matokeo sawa ya mabao 5-1. Mbili kati ya hizo zilijumuishwa na kusababisha kupoteza kwa jumla ya mabao 10-2 katika hatua ya 16 bora ya Ligi ya Mabingwa mwaka 2017.

Wakati huu, hata hivyo, hii si timu ya Arsenal katika hali mbaya ya utawala wa Arsene Wenger au timu ya Bayern katika kilele cha nguvu zao.

Ni upuzi kuipuuza Bayern katika hatua yoyote ya Ligi ya Mabingwa. Wamekuwapo kwenye eneo hili mara nyingi kabla na pamoja na Harry Kane, bado wana uzoefu wa kipa Manuel Neuer, mkongwe Thomas Muller na Joshua Kimmich na Leon Goretzka.

Kane anasaidiwa katika mashambulizi na kasi na tishio ya Leroy Sane, Jamal Musiala na Serge Gnabry.

Hata hivyo, Arsenal wanazidi kujiamini wanaposimama kileleni mwa Ligi Kuu England na kutafakari robo fainali yao ya kwanza baada ya miaka 14.

Kikosi cha Arteta kinaweza kuwa aina ambayo Bayern wanaweza kuhangaika nayo kutokana na kasi ya kusongesha mpira. Ni kazi ngumu lakini wana uwezo wa kushinda.

Washikabunduki, iwapo watashinda, basi watakabiliwa na mtihani mkubwa zaidi wa kucheza mechi mbili katika nne za mwisho dhidi ya Manchester City au Real Madrid. Lakini tumeona hapo awali kwamba hatua za mwisho mara nyingi hutoa hadithi zisizotarajiwa na Arsenal wanaweza tu kuanza kufikiria nafasi yao ya kuwa mmoja wao.

### Je, Mbappe ataondoka PSG akiwa na taji la Uefa?

Kylian Mbappe anacheza siku za mwisho za mkataba wake kule Paris St-Germain kabla ya kuhamia klabu nyingine majira ya joto, huku ikidhaniwa kuwa klabu hiyo itakuwa Real Madrid.

Hii inaweka matarajio ya kuvutia ya mchezaji huyo aliyeorodheshwa kuwa mchezaji bora zaidi duniani anayeweza kujaribu kuwanyima waajiri wake wa baadaye nafasi ya kushinda heshima kuu ya klabu ya soka ya Ulaya kwa mara ya 15 itakayoongeza rekodi na kocha wake wa baadaye Carlo Ancelotti ushindi wa tano wa ajabu katika mashindano hayo. Kuna uwezekano klabu zinaweza kukutana kwenye fainali huko Wembley.

Wachezaji nyota kama Mbappe, mshindi wa Kombe la Dunia akiwa na Ufaransa mwaka 2018, wanapata msukumo mkubwa zaidi kutokana na michezo hiyo mikubwa na nafasi ya kudai zawadi kubwa zaidi.

PSG, kwa gharama kubwa katika miaka ya hivi karibuni, wamekatishwa tamaa katika Ligi ya Mabingwa. Wametinga fainali mara moja tu, na kufungwa na Bayern Munich mnamo 2020.

Ikiwa Mbappe anataka kuwaachia kitu mashabiki wa PSG wamkumbuke kwa njia gani kwa kuweka historia kwa klabu?

PSG haizingatiwi kuwa miongoni mwa wanaopewa nafasi kubwa ya kutwaa kombe hilo na mechi yao ya nane ya mwisho dhidi ya Barcelona ya mpito itakaribia kuisha.

Watakuwa na matumaini ya ushindi, ingawa, ambayo itawaletea nusu fainali dhidi ya Atletico Madrid au Borussia Dortmund.


Litakuwa jambo la kushangaza ikiwa vijana wa Luis Enrique wangejiondoa, lakini kwa Mbappe lolote linawezekana - kwani atajaribu kuthibitisha kabla ya kuondoka.

## Nukuu

"Ingawa Arsenal wako kileleni, kwa mtazamo wa Liverpool, ningependelea kuwaona [The Gunners] wakienda kushinda Etihad au sare. Hakika si City kushinda kwa sababu kwa mechi tano za mwisho za City msimu huu, ungeweza kuwaangalia na ufikiri watapata pointi zote," **Nyota wa zamani wa Liverpool, Jamie Carragher.**



"Ukiangalia vizuri, kama [Kylian] Mbappe akienda Real Madrid, watakuwa na timu ambayo inaweza kutawala Ulaya na La Liga labda kwa miaka sita au saba kwa sababu wote watakuwa vijana, Mbappe, Vinicius, Rodrygo, Valverde, Tchouameni," **Nyota wa zamani wa Arsenal, Barcelona na Ufaransa, Thierry Henry.**



"Arsenal. Unapaswa kusema Arsenal. Kilichotokea msimu uliopita, wanajua nini cha kufanya. Wachezaji wote wako fiti sasa. Sitakaa hapa sema, 'natumai'. Hapana kwa sababu sivyo unavyotaka. kusikia. Hicho sicho kile wachezaji wanachofikiria. Ni timu yenye uhusiano mkali sana, meneja anatamani sana, bila shaka, nitasema Arsenal, lazima." **Nguli wa zamani wa England, Ian Wright, akitabiri kuhusu timu itakayotwaa ubingwa wa Ligi Kuu nchini humo kati ya Arsenal, Liverpool na Manchester City.**





Msikiti wa Masjid Samatta. **PICHA: SAADA AKIDA**

# SAMATTA ANAVYOREJESHA KWA JAMII KAMA MANE

**Na Saada Akida**

MSHAMBULIAJI wa Al Nassr ya Saudi Arabia, Sadio Mane, ambaye kabla ya kujiunga na timu hiyo alipata mafanikio makubwa akiichezea Liverpool ya England kabla kutimkia Bayern Munich ya Ujerumani, ni miongoni mwa wachezaji wachache wa Afrika wanaojitoa kwa jamii kwa kujitolea kusaidia mambo mbalimbali.

**Machache kati ya mengi aliyofanya Mane ni pamoja na kujenga uwanja mkubwa wa kisasa wa soka kijijini kwao, lakini pia akijenga shule za kisasa na hospitali kubwa na siku zote anasema moyoni mwake anafikiria ni namna gani ataweza kuwasaidia zaidi watu wa Senegal.**

Ni wanasoka wachache wamekuwa wakijitoa kwa kurejesha katika jamii zao kile wanachokipata, kama ilivyo kwa Mane, mwanasoka wa Tanzania Mbwana Samatta, anayeichezea Klabu ya PAOK ya Ugiriki, naye ameguswa na kuona umuhimu kufanya jambo kubwa kwa jamii inayomzunguka ambapo Ijumaa ya Machi 8, mwaka huu, ulizinduliwa rasmi msikiti aliougharamia kwa fedha zake mwenyewe ukiwa na uwezo wa kuingia waumini 15,000 kwa wakati mmoja.

Msikiti huo uliopewa jina la Masjid Samatta. Upo Vikindu Wilaya ya Mkuranga mkoani Pwani, ambapo baba mzazi wa nyota huyo, Ally Pazi Samatta aliukabidhi rasmi kwa wakazi wa eneo hilo.

Ni Samatta ambaye alianzia soka lake katika Klabu ya Kimbangulile, Mbagala Market kisha African Lyon, Simba, TP Mazembe ya Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo, KRC Genk ya Ubelgiji na Aston Villa ya England, Galatasaray ya Uturuki na sasa PAOK.

Nipashe lilifanikiwa kutembelea maeneo ya msikiti huo na nyumbani kwa baba mzazi wa nahodha huyo wa Timu ya Taifa, Taifa Stars kuzungumza mambo mbalimbali ikiwamo wazo lake la kujenga msikiti huo.

## MSIKITI UMEKAMILIKA

Mzee Samatta anasema, ana furaha kubwa kuona kijana wake amerudisha shukrani kwa Mungu na jamii, anaamini kupitia hilo ataendelea kupata baraka kwenye jukumu lake kama mwanasoka.

"Ni jambo jema kumkumbuka Muumba kwenye ujana wake, pamoja na neema anazozipata maishani mwake bila Mungu ni bure, ndio maana akiniambia anataka kufanya vitu vya huduma kwa wengine na kuwa mstari wa mbele kuvisapoti," anasema Mzee Samatta na kuongeza

"Samatta si muongeaji, lakini anajitoa sana kwa jamii bila kubagua, hilo linanigusa kama mzazi, kuna wengine nimewasikia wakisema sasa angekujengea ghorofa, nawaambia ninalo la kwangu nililojenga kwenye ujana wangu, hivyo anachokifanya ni bora zaidi."



Mwandishi wa Nipashe, Saada Akida, alipomtembelea Mzee Ally Pazi Samatta, kufanya naye mazungumzo maalum wiki iliyopita. **MPIGAPICHA WETU**

## UJENZI ULIVYOANZA:

Baba mzazi wa mchezaji huyo anasema kuna siku alitoka Vikindu ambapo kuna viwanja vyake wakati huo Samatta akiwa anacheza TP Mazembe ya DR Congo.

"Nakumbuka ilikuwa mwaka 2017 aliporudi Congo akanieleza anataka kununua viwanja Vikindu kwa ajili ya kujenga nyumba yake ya makazi, nilifanikiwa hilo kwa kupata viwanja hivyo na kununua, lakini baada ya muda mfupi alinifuata na kunieleza amepata kiwanja Kigamboni anataka kununua.

"Nilimkubalia kwa bahati nzuri aliponunua Kigamboni akapata wazo la kujenga nyumba ya kuishi huko na kunieleza kuwa kiwanja cha Vikindu anataka kujenga msikiti.

"Nilimuunga mkono kwa sababu amefuata nyayo za babu yake mmoja anaitwa Mbwana Samatta alijenga nyumba ya ibada huko Bagamoyo," anasema Mzee Samatta.

Anaelezea kuwa baada ya kuona sijampinga wazo lake akaanza ujezi kwa haraka, umechukuwa muda wa miaka mitatu ujezi ukasimama kwa sababu ya piLika za usajili wake wa kwenda Aston Villa.

Anasema baada ya kusimama mwaka 2023 wakazi wa Vikindu walimfuata kuomba idhini ya kutaka kutumia msikiti huo, ambapo aliwaeleza hujakamilika ikiwamo kutokuwapo maji pamoja na kutopakwa rangi.

"Waliniomba kutumia hivyo hivyo hadi hapo tutakapokuwa tayari na tukawaruhusu kutumia wakati ujezi ukiendelea hadi umekamilika na kufunguliwa," anasema baba mzazi wa Samatta.

Msikiti huo wa Samatta ulianza kujengwa mwaka 2017 na Mzee Samatta anasema ameona kama ametua mzigo kwa kuzinduliwa na kuanza kutumika na roho yake ina amani kubwa.

"Thamani halisi ya msikiti huo hajaiwekwa wazi kutokana usiri mkubwa ambao anao kijana wangu, ni kuwa msiri katika mambo yake mengi," anasema mzee Samatta ambaye enzi za ujana wake naye alikuwa mahiri katika soka kama ilivyo kwa mwanawe.

## JAMII ANAYOISAIDIA

Mzee Samatta anaeleza kuwa mbali na msikiti huo pia anawadhamini watoto yatima katika vituo viwili (majina hayafahamu), vilivyo Kinondoni na kingine Bagamoyo kwa kuwapa vitu vyote vya msimgi ambavyo wanatakiwa kupata kutoka kwa wazazi au walezi wao.

"Mwaka jana katika mashindano aliyoyaanzisha yeye na Ali Kiba (Samakiba Foundation), alitoa milioni 100 kwa ajili ya kununua vifaa vya akina mama wanaojifungia watoto njiti katika Hospita ya Kibiti ambapo nimezaliwa baba yake," anasema mzee Samatta.

## VITEGA UCHUMI VYAKE

Baba mzazi wa nyota huyo anasema Nahodha huyo wa Taifa Stars amekuwa na biashara nyingi ikiwamo Samatta Safari Tours kwa ajili ya usafirishaji wa watalii kwenda kutembelea mambo ya kitalii.

"Hajaishia hapo lakini aliniambia anamipango ya kumiliki TV yake kwa ajili ya michezo tu, lakini hajaweka wazi juu ya atakapomaliza soka lake anahitaji kufanya nini."

## AMGOMEA SAMATTA:

Anasema kipindi ambacho Samatta amemaliza nyumba yake, kijana wake alimtaka akaishi Kigamboni, lakini alimgomea kwa sababu hawezi kukaa sehemu ambayo haina makelele wala fujo.

"Nilimkatalia nikamwambia hawezi kuniamisha Mbagala na kwenda kunifungia Kigamboni hutoki nje muda wote ndani hayo maisha ya kizungu siyawezi nimezoea kwangu hapa Mbagala muda wote fujo kelele na kutoka kwenda katika viwanja mbalimbali kuangalia mpira," anasema Mzee Samatta.

## JE, WAJUA?



KWA mujibu wa nguli wa zamani wa Arsenal, Paul Merson, ambaye aliichezea mechi 327 na kuifungia mabao 78, makocha watatu bora kwake wa wakati wote kwenye Ligi Kuu England ni Sir Alex Ferguson, Jose Mourinho na Arsene Wenger.



# RC Dendego avalia njuga matumizi vyoo bora

**Na Thobias Mwanakatwe,** MANYONI

KUTOKANA na Mkoa wa Singida kuwa na kiwango kidogo cha matumizi ya vyoo, Mkuu wa Mkoa wa Singida, Halima Dendego, amewaagiza viongozi kuhakikisha kila kaya inakuwa na choo bora ili kujiepusha na magonjwa ya mlipuko.

Akizungumza juzi katika kikao kazi cha viongozi wa serikali na Chama Cha Mapinduzi (CCM) wilayani Manyoni, Dendego alisema kutotumia vyoo kunaondoa ustaarabu na kuchafua mazingira hali inayohatarisha afya zao kupata magonjwa ya mlipuko kama kipindupindu.

Dendego alisema katika utendaji kazi wake atapenda, kuwashirikisha na kuwaheshimu watu wote na kama kiongozi kuna sehemu lazima atakaza kamba lakini sio kwa nia mbaya bali ni kuhakikisha wanafikia malengo yaliyokusudiwa.

Alisema serikali imekabidhiwa kuuza duka na CCM hivyo ni lazima kuwapa hesabu iliyokamilika ambayo haina mashaka ili kuwawezesha viongozi kutembea kifua mbele wakati wa kwenda kuomba ridhaa kwa wananchi na kuweza kupata kibali cha kuongoza miaka mitano mingine.

"Nitawashirikisha sana kwenye vikao chama na Serikali na tukitoka kule nje wote tunakuwa tunaimba wimbo mmoja, ukitaka upate wimbo ulio bora ni ushirikishwaji, shindaneni kwenye vikao lakini fanyeni maazimio ya pamoja na wote mkitoka pale mtaona njia iliyonyooka," alisema.

Akizungumzia suala la usalama wa chakula aliagiza kila kata kuhakikisha inasimamia mazao yanastawi ili wananchi wajitosheleze kwa chakula.

Alisema ni lazima Singida ifanye mapinduzi ya kilimo, kwani serikali imeleta mbolea ya ruzuku ili wananchi waitumie kwa lengo la kupata mavuno maradufu. "Nimetoka Iringa ya kijani nataka Singida ya kijani na kimsingi nimeona mnachukua hatua lakini tutapambana kufikia malengo kwa kuzalisha chakula cha kutosha," alisema.

Kuhusu elimu, Dendego alisema shule za sekondari zinazojengwa na serikali lengo ni kuhakikisha zinakuwa na wanafunzi wa kutosha, hivyo jitihada zifanyike kuongeza ufaulu wa wanafunzi wa darasa la saba na kwamba ifikapo Desemba mwaka huu ifike asilimia 90 ya lengo kwa kila sekta.



Mkuu wa Mkoa wa Singida, Halima Dendego akifungua bomba jana kuangalia kama maji yanatoka katika kioski kilichopo kijiji cha Maweni wilayani Manyoni ambacho kimejengwa kupitia Mradi wa maji wa Kintinku-Lusilile ambao utakapokamilika zaidi ya wakazi 55,000 wa vijiji 11 wilayani humo watanufaika, utagharimu Sh.bilioni 13 hadi kukamilika. **PICHA: THOBIAS MWANAKATWE.**

# NBC yajivunia mikopo bil. 28/- kwa wateja 20,000 ikifuturisha

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

BENKI ya Taifa ya Biashara (NBC) imeandaa futari mahususi kwa wateja wake wa Kiislamu jijini Dodoma huku ikijivunia mafanikio makubwa katika utoaji mikopo kupitia huduma yake maalum kwa wateja wa Kiislamu inayojulikana kama La Riba, inayozingatia mafundisho ya Kiislamu kuhusu riba.

Hafla hiyo ilifanyika mwishoni mwa wiki jijini hapa, ikiongozwa na Katibu Mkuu wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Ally Gugu aliyemwakilisha Waziri Yusuf Hamad Masauni.

Mkurugenzi wa Mikopo wa NBC, Salehe Mohammed alimwakilisha Mkurugenzi Mtendaji wa benki hiyo, Theobald Sabi kwenye hafla iliyohudhuriwa pia na wageni mbalimbali waalikwa wakiwamo wateja na viongozi waandamizi serikalini akiwamo Mkuu wa Wilaya ya Dodoma, Jabir Shekimweri aliyemwakilisha Mkuu wa Mkoa huo, Rosemary Senyamule pamoja na Mkuu wa Wilaya ya Chemba, Gerald Mongela.

Akizungumza kwenye hafla hiyo, Salehe alisema tangu kuanzishwa huduma ya La Riba, tayari jumla ya Sh. bilioni 28 imetolewa kwa wateja zaidi 20,000 katika maeneo mbalimbali nchini.

"Kimsingi ni kwamba kumekuwa na mwitikio mzuri kutoka kwa wateja kuhusiana na huduma yetu ya La Riba inayozingatia misingi ya dini ya Kiislamu katika masuala ya riba na zaidi tunajivunia kuona kwamba huduma hii imejipambanua kama msaada mkubwa kwa wafanyabiashara na wajasiriamali wenye imani ya dini ya Kiislamu.

Katika hotuba yake kwenye hafla hiyo, Katibu Mkuu wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Gugu, alipongeza benki ya NBC kwa ushirikiano wake na wadau wake huku akisisitiza umuhimu wa huduma bora za kifedha zinazoheshimu imani za kidini katika kuchochea ukuaji wa uchumi wa taifa sambamba na kuleta utulivu na amani ya nchi.

"Ni wazi kwamba utoaji huduma za kifedha unaozingatia na kuheshimu imani za wateja sambamba na kufuata sheria ya nchi ni moja ya sababu muhimu inayochochea utulivu na amani ndani ya nchi kwa sababu watu wanaendesha shughuli zao wakijua wazi kile wanachokipata kinahifadhiwa sehemu salama na hata wanapohitaji huduma za kifedha ikiwamo mikopo pia wanaipata vizuri.

"Tena NBC mmeenda mbali zaidi ambapo kupitia huduma ya La Riba mnatoa mikopo kwa wateja wenye imani ya Kiislamu kwa kuzingatia mafundisho ya dini kuhusu suala zima la riba," alisema.

Mkuu wa Wilaya ya Dodoma, Shekimweri, alipongeza benki hiyo kwa kuandaa hafla hiyo aliyoitaja ni kuthibitisha dhamira ya benki hiyo katika kuwajali wateja wake, pia kutoa fursa kwa wateja hao kufurahi pamoja na kujenga uhusiano mzuri miongoni mwao na benki hiyo.

# Sheria kandamizi, uhaba malisho bado tatizo kwa wafugaji

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

IMEELEZWA kuwa wafugaji nchini bado wanakabiliwa na kero mbalimbali ikiwamo sheria kandamizi, uhaba wa malisho na migogoro baina yao na wakulima.

Mgombea wa nafasi ya Mwenyekiti wa Chama cha Wafugaji Tanzania (CCWT) Taifa, Simon Ndaki, alibainisha hayo jana jijini hapa, alipokuwa akieleza vipaumbele vyake atakavyo vifanyia kazi baada ya kuchukua fomu ya kuwania kiti hicho.

Alisema kutokana na kero hizo ambazo zinarudisha nyuma sekta ya mifugo amejipanga katika uongozi wake kushirikiana na wafugaji na serikali kuzipatia ufumbuzi.

Alisema kero nyingine atakayo ifanyia kazi ni sheria kandamizi ambazo zinapaswa kufanyiwa kazi ili kuondoa hali iloyopo hivi sasa ya kuwanyonya wafugaji.

Aidha, alisema kero nyingine ni ukosefu wa masoko ya uhakika ya bidhaa za mifugo nchini hali ambayo imekuwa ikichangia wafugaji kuendelea kuwa maskini.

Pia, alisema kama atapata nafasi hiyo atahakikisha anashirikiana na serikali kukomesha mauaji ya wafugaji yanayotokana na askari wa mapori ya hifadhi ya misitu kuwapiga risasi wanapo ingiza mifugo yao hifadhini.

Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi wa Chama cha Wafugaji CCWT, Charles Malagwa alisema hivi sasa wagombea mbalimbali wanachukua fomu kwa ajili ya uchaguzi ngazi ya taifa utakaofanyika Aprili 8, mwaka huu.

# Profesa Kitila ataja mafaniko matatu uongozi wa Samia

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, Prof.Kitila Mkumbo amesema miaka mitatu ya uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan kumekuwapo na ongezeko la uwekezaji, ajira na kiwango cha mtaji nchini.

Aliyasema hayo juzi wakati akizindua baraza la kwanza la wafanyakazi wa ofisi hiyo na kueleza kuwa kutokana na sera na maono yake yamechochea miradi 1,075 iliyosajiliwa ikilinganishwa na kipindi kama hicho kilichopita ambapo ilisajiliwa miradi 700.

"Katika uongozi wake ametengeza ajira kupitia uwekezaji 137,000 ikilinganishwa na kipindi cha miaka mitatu iliyopita zilikuwa takribani 80,000, huku mitaji imekuwa Dola za Marekani bilioni 14.2 ikilinganishwa na kipindi kilichopita ilikuwa Dola za Marekani bilioni 6.1,"alisema.

Aidha, alisema katika sekta ya mipango na uwekezaji Rais Samia amekuwa ni Rais wa pili kupata fursa ya kuandika dira tangu nchi ipate uhuru.

Akizungumzia kuhusu baraza hilo, Prof.Mkumbo aliwaasa wafanyakazi kujiepusha na utamaduni wa kuogopa viongozi kwa kuwa unahatarisha utendaji wa taasisi.

Pamoja na hayo, aliwaasa katika maisha ya utumishi wa umma wasitafute vyeo kwa nguvu bali waache vyeo viwafuate.

Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Dk.Tausi Kida, alisema baraza hilo ni muhimu katika kusimamia maslahi ya wafanyakazi na kushauri ofisi kubuni sera zitakazowavutia wawekezaji.



# Konokono wavamia mashamba, waharibu mazao

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WADUDU aina ya konokono wamevamia mashamba ya wakulima katika kata tatu za Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya na kuharibu mazao, hali ambayo inahatarisha usalama wa chakula na uchumi wa wananchi hao.

Kata zilizoathirika na uvamizi wa wadudu hao ni Utengule, Mshewe na Igale ambazo ni miongoni mwa kata zinazozalisha chakula kwa wingi katika halmashauri hiyo.

Wakizungumza na Nipashe wananchi wa maeneo hayo walisema wadudu hao hawajulikani walikotokea na wanashambulia mazao kwa kasi na hawafi kwa sumu yoyote, hali ambayo inawapa wasiwasi kwamba huenda wakakumbwa na baa la njaa na kushuka kiuchumi.

Mmoja wa wananchi hao, George Mwasenyanga ambaye ni mkazi wa Kijiji cha Njelenje kilichopo Kata ya Mshewe alisema wadudu hao wamekuwa wakiwasumbua kwa zaidi ya miaka mitano sasa na wamekuwa wakijaribu kila aina ya sumu lakini hawafi.

Alisema wadudu hao wanaharibu mazao kama maharage, mahindi, alizeti na kahawa kwa kuyakata shina yakiwa machanga, kula majani na kulamba matunda hali ambayo inasababisha mavuno kuzorota. "Awali walikuwa wanakula maharage, alizeti na kahawa lakini kwa sasa wanashambulia mpaka mahindi, wanalamba majani yakiwa madogo na hivyo kuufanya mmea kushindwa kuendelea, tunaiomba serikali itusaidie kukabiliana nao maana hawafi kwa sumu yoyote," alisema Mwasenyanga.

Mzee Godwin Matapila alisema wadudu hao miaka ya nyuma walikuwepo lakini walikuwa hawaharibu mazao kama ilivyo sasa na kwamba hawaelewi sababu ya kubadilika tabia kwa wadudu hao na kuanza kuharibu mazao.

Alisema miaka ya nyuma walikuwa wakiwakuta shambani walikuwa hawahangaiki nao kutokana na kutokuwa na madhara yoyote lakini kwa sasa wamekuwa kero na wanawaingiza hasara.

Alisema tatizo kubwa lipo kwenye mazao jamii ya mikunde na kahawa ambayo ndiyo yanayoshambuliwa zaidi kuanzia yanapopandwa mpaka yanapokomaa na kwamba mahindi yanashambuliwa yakiwa machanga lakini majani yakikomaa wanaacha kula. "Katika umri wangu sijawahi kufikiri kwamba konokono wanaweza wakaharibu mazao, wadudu hawa wanazaliana kwa kasi kubwa sana kiasi kwamba hata kuwakabili inakuwa ngumu," alisema Mwatapila.

Naye Safia Songolo alisema wamekuwa wakifanya kazi ya kuwaokota konokono hao mashambani na kuwaweka kwenye mifuko kisha kuwaua kwa kuwamwagia chumvi, majivu ama mbolea kisha kuwatupa. Alisema baadhi wamekuwa wakiwaokota na kuwakusanya kisha kuwafukia chini ya ardhi ama kuwafunga kwenye mifuko aina ya nailoni ili wakose hewa na wafe.

Alisema shughuli ya kuwaokota ni ngumu hasa kwa watu wenye mashamba makubwa na hivyo akaiomba serikali kuwasaidia namna sahihi ya kukabiliana nao.

Ofisa Kilimo wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, Obel Kasamale ambaye anasimamia kahawa katika halmashauri hiyo alisema baada ya kukithiri kwa wadudu hao waliamua kuanza kuwasiliana na taasisi mbalimbali za serikali ili kusaidiana kuwakabili.

Alisema walishatoa taarifa kwenye Mamlaka ya Afya ya Mimea na Viuatilifu (TPHPA), Bodi ya Kahawa nchini pamoja na Taasisi ya Utafiti wa Kahawa nchini (TCRI).



Naibu Waziri wa Maji, Maryprisca Mahundi (kushoto) akimkabidhi Meneja wa Wakala wa Usambazaji wa Maji Safi na Usafi wa Mazingira vijijini (RUWASA) Wilaya ya Mbarali, Samwel Echey nyaraka za uchimbaji wa visima katika kata tano za Wilaya ya Mbarali mwishoni mwa wiki alipozindua uchimbaji wa visima hivyo katika kijiji cha Azimio-Mpula. **PICHA: NEBART MSOKWA.**

# Dereva wa bodaboda auawa na aporwa

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

MKAZI wa mtaa wa Matema Kata ya Maguvani Halmashauri ya Mji wa Makambako mkoani Njombe, Titus Pelamiho (38) ameuwawa kwa kukatwa na kitu chenye ncha kali kichwani na katika sikio.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Njombe, Kamishna Msaidizi Mahamoud Banga aliyasema hayo juzi na kueleza kuwa tukio hilo lilitokea machi 20 mwaka huu majira ya saa 2:00.

Kamanda Banga alisema bodaboda huyo alikutwa kwenye Mtaa wa Matema akiwa ameuawa kwa kukatwa na kitu chenye ncha kali maeneo ya kichwani na kwenye sikio la upande wa kulia

"Marehemu alikuwa ni dereva wa pikipiki ambayo imechukuliwa na watu wanaodaiwa kutekeleza mauaji hayo," alisema Banga.

Alisema katika tukio hilo Jeshi la Polisi linaendelea na uchunguzi na watuhumiwa wawili wanashikiliwa na jeshi hilo na wanaendelea kuwahoji.

"Pikipiki hiyo iliyochukuliwa thamani yake ni Sh. milioni 2.7, katika tukio hili tunaendelea na uchunguzi watu wawili tumewakamata" alisema Kamanda Banga. Mwenyekiti wa Mtaa wa Matema, Thomson Mathai Nziku alisema alipigiwa simu na balozi wa eneo hilo ambapo alichukua uamuzi wa kwenda kushuhudia lakini baada ya kufika hapo alifanikiwa kuukuta mwili wa marehemu huyo ukiwa katika eneo hilo.

"Ninatoa angalizo kwamba boda boda wawe makini anapoondoka kuelekea mahali hasa wakati wa usiku wahakikishe anakuwa na mtu anafuatana nae maana hatujui mtu anayemchukua ni mwema au siyo mwema," alisema Nziku.

Mwenyekiti wa Chama cha Madereva wa Bodaboda Halmashauri ya Mji wa Makambako, Yusuph Mtelesi alisema tukio hilo limetokea usiku wa kuamkia machi 20 mwaka huu na marehemu alikuwa mwanachama wao.

"Tunachotambua sisi mwenzetu ameuawa ila ameuawa na nani hatufahamu, lakini ni kweli dereva boda boda mwanachama wetu na alijiunga Januari mwaka jana," alisema Mtelesi.

Aliwataka madereva wa boda boda Halmashauri ya Mji wa Njombe kudumisha umoja wao ili kuepuka matukio ya mauaji kwani kunapotokea migogoro wahalifu ndiyo wamekuwa wakitumia nafasi hiyo kufanya mauaji.

# Waliokuwa wanatumia maji ya mtoni sasa kuchimbiwa visima

**Na Nebart Msokwa,** MBARALI

WANANCHI kutoka kata sita za Wilaya ya Mbarali wanatarajia kuondokana na tatizo la kutumia maji ya kwenye mito na madimbwi baada ya serikali kuanza kuchimba visima kwa ajili ya kuwasambazia maji.

Kata ambazo zitanufaika na visima hivyo ni pamoja na Kongolo-Mswiswi, Utengule-Usangu, Ipwani, Miyombweni, Ubaruku na Igava ambazo zimekuwa zikikabiliwa na tatizo la huduma hiyo kwa muda mrefu.

Wakizungumza mwishoni mwa wiki wakati wa uzinduzi wa uchimbaji wa visima hivyo katika Kijiji cha Azimio- Mpula kilichopo Kata ya Kongolo-Mswiswi, wananchi hao walisema wamekuwa wakitumia maji ambayo usalama wake ni wa mashaka.

Mmoja wa wananchi hao, Kunji Shimbi alisema walikuwa wanapata shida zaidi kipindi cha kiangazi ambapo mito mingi wilayani humo ambayo ni ya msimu inakuwa imekauka na kwamba wamekuwa wakitembea umbali mrefu kwenda kufuata huduma hiyo.

Alisema wamekuwa wakifukua visima vidogo kwenye mchanga na kusubiri maji yatwame ndipo wachote hali ambayo imekuwa ikiwasababishia kutumia muda mwingi kutafuta huduma hiyo.

Alisema maji hayo ambayo wamekuwa wakiyatumia hawana uhakika na usalama wake kutokana na wanyama mbalimbali pia kuyatumia.

"Tunaishukuru sana serikali kwa uamuzi huu wa kutuletea mradi wa kisima kirefu, maji tuliyokuwa tunatumia kwa sehemu kubwa ni machafu, tulikuwa tunasubiri yajichuje kwenye mchanga ndipo tutumie na yalikuwa yanakuwa na rangi utafikiri maziwa," alisema Kunji.

Mariam Katanta alisema wakati mwingine wamekuwa wakiumwa matumbo bila kujua sababu na kwamba yeye binafsi anahisi chanzo ni maji ambayo wamekuwa wakiyatumia hasa kunywa kwa maelezo kuwa hali hiyo hupungua kipindi cha mvua.

Alisema kipindi cha masika wamekuwa wakichota maji ya mvua kwa kukinga kwenye nyumba zao na kwamba wakati huo huwa hawapati shida ya kuugua matumbo kama inavyokuwa kiangazi.

Alisema baadhi ambao wana vyombo vingi vya kuhifadhia maji wamekuwa wakichota ya mvua na kuyahifadhi kwa ajili ya kuyatumia kiangazi.

Mwenyekiti wa Ustawi wa Jamii wa Kijiji cha Azimio-Mpula, Frank Nguvila alisema wanawake wa kijiji hicho wamekuwa wakipata shida ya maji kwa kutembea umbali mrefu kwenda kutafuta huduma hiyo.

Alisema kijiji hicho miaka ya nyuma kiliwahi kuwa na visima viwili vya kuvuta lakini kwa miaka ya sasa havitoi maji kutokana na mabadiliko ya tabianchi.

Alisema kitendo cha serikali kuwapelekea mradi wa kisima kitawasaidia kuondokana na tatizo la uhaba wa maji na hivyo muda waliokuwa wanautumia kutafuta maji umbali mrefu watautumia kwenye shughuli zingine za uzalishaji.

Meneja wa Wakala wa Usambazaji wa Maji Safi na Usafi wa Mazingira vijijini (RUWASA) Wilaya ya Mbarali, Samwel Echey alisema mradi huo unalenga kutatua kero ya maji kwenye vijiji 23 vya wilaya hiyo ambavyo havina maji.

Alisema kisima kimoja kinagharimu zaidi ya Sh. milioni 500 ikiwa ni pamoja na gharama za usambazaji wa maji hayo kwa wananchi pamoja na ujenzi wa vituo vya kuchotea maji.

Alisema kila kata zinazonufaika na mradi huo zinachimbiwa kisima kimoja kwenye eneo ambalo limefanyiwa utafiti.

Akizindua uchimbaji wa visima hivyo, Naibu Waziri wa Maji, Maryprisca Mahundi alisema serikali imenunua mitambo 25 na kuisambaza kwenye mikoa yote kwa ajili ya kuchimbia visima ili kukabiliana na tatizo la uhaba wa maji.

Hivyo, aliwataka wasimamizi wa mitambo hiyo kuitumia vizuri na kuhakikisha inafanya kazi ambayo inakusudiwa ili itumika muda mrefu na kutatua kero ya maji kwa wananchi.



# Idadi ya wageni wanaoingia Zanzibar yashuka

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

IDADI ya wageni walioingia Zanzibar katika kipindi cha Februari mwaka huu ni 71,095, ikiwa ni ndogo kulinganisha na kipindi cha Januari waliokuwa 73,468.

Mtakwimu kutoka Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali Zanzibar, Khamis Abrahman Msham, alieleza hayo jana alipokuwa akiwasilisha takwimu za uingiaji wageni kwa kipindi cha Februari.

Alisema wageni walioingia Februari mwaka huu walikuwa ni 71,095 ambapo Ulaya iliongoza kuwa na wageni wengi zaidi ambao ni 58,735 sawa na asilimia 82.6.

Alisema bara lilofuatia kwa kuleta wageni wengi ni Afrika ambalo lilikuwa na wageni 4,932, Asia wageni 3,602 sawa na asilimia 5.1 na Oceania wageni 381 sawa na aslimia 0.5.

Msham alisema nchi tano zilizoongoza kwa kuwa na wageni wengi waliofika Zanzibar ni Italia ilikuwa na wageni 9,695 sawa na asilimia 13.6 ya wageni wote ikifuatiwa na Ufaransa 8,771 sawa na asilimia 12.3, Poland wageni 6,938 sawa na asilimia 9.8, Ujerumani 5,806 sawa na asilimia 8.2 na Scandivavia 3,611 sawa na asilimia 5.1.

Alisema wageni 63,242 sawa na asilimia 89.0 ya wageni waliongia Zanzibar walitumia usafiri wa anga kupitia viwanja vya ndege na wageni 7,853 sawa na asilimia 11.0 walitumia usafiri wa maji kwa kutumia boti kupitia Bandari ya Malindi.

Alisema idadi yote ya wageni waliofika Zanzibar kwa mwezi huo wa Febuari wanawake walikuwa wengi zaidi ambao ni 38,724 sawa na asilimia 54.5 ikilinganishwa na wanaume ambao walikuwa 32,371 sawa na asilimia 45.5.

# Wasindikaji vyakula wasimulia walivyoyafikia masoko Ulaya

**Na Mwandishi Wetu**

WASINDIKAJI wa vyakula walio chini ya Mradi wa AINFP- Technoserve uliomaliza muda wake, wameeleza namna elimu ya usindikaji waliyopata ilivyowawezesha kuuza bidhaa zao katika masoko ya kimataifa.

Wakizungumza juzi katika kongamano la kumaliza mradi huo baadhi ya wasindikaji walisema umewaunganisha na masoko ya ndani na nje ya nchi.

Mkurugenzi Mtendaji wa NatureRipe, Fatma Riyami, alisema mradi huo umemwezesha kumuunganisha na masoko ya kimataifa katika nchi mbalimbali.

Alisema waliwaomba Technoserve kuwasaidia namna ya kufungasha bidhaa zao na kuwa na ubora wa muda mrefu, ndipo walipowapatia wataalam kutoka Marekani ambao kufanya nao kazi tangu 2018.

Shela Milanzi wa kampuni ya Shamba Milk kutoka mkoani Morogoro wanaojihusisha na uzalishaji wa bidhaa za maziwa, alisema wamenufaika na utaalam ikiwamo usindikaji na njia ya kulifikia soko.

Mkurugenzi wa Mradi wa AINFP, Angela Mupaisho, alisema mradi huo ulihusisha nchi za Ethiopia, Malawi, Kenya, Tanzania na Zambia na umewawezesha wasindikaji kuongeza mauzo na kuwa washindani sokoni.

Meneja wa mradi wa AINFP-Tanzania, Getrude Kawawa, alisema mradi huo umetekelezwa Tanzania takribani miaka sita kwa kufanya kazi na wasindikaji wa vyakula.

Kadhalika alisema wamewasaidia katika masuala ya kupatikanaji wa fedha kwa kuwaunganisha na taasisi za fedha ambapo wengi wao wamepata mikopo inayofikia Dola za Marekani milioni 2.5 katika kuendeleza biashara zao.

Ofisa Kilimo Mkuu wa Mamlaka ya Udhibiti wa Nafaka na Mazao Mchanganyiko Tanzania (COPRA), Marry Majule, alisema kupitia mradi huo wasindikaji waliopata utaalamu wa kiufundi ni 51, kati yao wanawake ni 33.

# NMB yawaandalia futari yatima na wanaoishi mazingira magumu

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

BENKI ya NMB imeendeleza utamaduni wa kufuturisha wateja wake walioko kwenye Mfungo wa Mwezi Mtukufu wa Ramadhani baada ya kufanya hafla mbili tofauti za Iftar katika visiwa vya Unguja na Pemba mwishoni mwa wiki.

Mgeni rasmi alikuwa Makamu wa Pili wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ), Hemed Suleiman Abdulla.

Makamu wa Pili wa Rais alihudhuria hafla iliyofanyika Alhamisi mjini Unguja, ambako NMB iliongozwa na Ofisa Mtendaji Mkuu (CEO), Ruth Zaipuna na Mwenyekiti wa Bodi ya NMB, Dk. Edwin Mhede huku Mkuu wa Mkoa wa Kusini Pemba, Mattar Zahoro Masoud, akiwakilisha SMZ katika Iftar ya Pemba.

Katika hafla hizo mbili, NMB ilifuturisha takribani waalikwa 1,000, wakiwamo wateja, wadau viongozi wa SMZ pamoja na watoto yatima na wanaoishi kwenye mazingira magumu. Kati yao, waalikwa karibu 600 walihudhuria hafla ya Unguja na wengine wapatao 400 walijumuika pamoja Kisiwani Pemba.

Mjini Unguja, Makamu wa Pili wa Rais alisema SMZ inapongeza NMB kwa kudumisha utamaduni huo na inatambua na kuthamini mchango wa taasisi hiyo katika maendeleo visiwani humo, huku akisema siri ya mafanikio ya ongezeko la mapato Zanzibar ni ushirikiano wa kimfumo baina ya benki hiyo na serikali yake.

"Niwahakikishie kwamba tutaendelea kuimarisha mifumo kupitia NMB, kwani ninaelewa kuwa kuna kazi kubwa sana za SMZ mmezifanya na zimetusaidia sana na hapa nikiri kwamba ongezeko la makusanyo ya mapato ya Serikali ya Zanzibar, moja ya siri za mafanikio hayo ni mchango wa NMB," alisema.

Aliongeza kwa kutoa ahadi, akisema SMZ itaendelea kuwapa NMB ushirikiano na kuwa pamoja nao katika hali zote, ili kuhakikisha benki hiyo inafanya kazi zake kwa ufanisi.

Mbali na Makamu wa Pili wa Rais, hafla hiyo pia ilihudhuriwa na mawaziri, wabunge na wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, wakiwamo Waziri wa Uchumi na Uwekezaji Zanzibar, Sharif Ali Sharif na Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji na Mifugo Zanzibar, Shamata Shaame Khamis.

Awali, Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya NMB, Zaipuna, alikiri kuwa kusanyiko hilo ni faraja kubwa kwa NMB kujumuika pamoja na wananchi wa Zanzibar, hususani wateja wa benki yake walio kwenye mfungo wa Mwezi Mtukufu wa Ramadhani, wadau na viongozi wa serikali.



Makamu wa Pili wa Rais Zanzibar, Hemed Suleiman Abullah (mwenye koti jeusi) akikabidhi msaada wa vyakula kwaajili ya Futari kwa watoto waishio katika Mazingira magumu uliotolewa na Benki ya NMB wakati wa futari iliyoandaliwa na Benki hiyo Visiwani Zanzibar. Kushoto ni Meneja wa Biashara za Zanzibar wa Benki ya NMB, Naima Said Shaame, wapili kushoto ni Afisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya NMB, Ruth Zaipuna, kulia na Mwenyekiti wa Bodi ya wakurugenzi ya Benki ya NMB, Dk. Edwin Mhede na wengine ni watoto kutoka vituo vililivyopokea msaada huo. **PICHA: MPIGAPICGA WETU**

# ZEEA yawawezesha vijana kuibua miradi, kujikwamua

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

IMEELEZWA kuwa kuanzishwa kwa Wakala wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi Zanzibar (ZEEA), ni fursa muhimu ya kuwawezesha vijana kuibua miradi katika kazi za ubunifu na kupata fedha za kuendeleza kazi zao za kujikwamua kiuchumi.

Hayo yalisemwa juzi na Mkurugenzi Mkuu wa ZEEA, Juma Burhani wakati akifunguwa mafunzo katika mradi wa "Tanzania imarisha sekta binafsi".

Mkurugenzi huyo aliwataka vijana kujitokeza kuchangamkia fursa za ujasiriamali kwa ajili ya kuibuwa miradi ambayo itawawezesha na kuwainuwa kiuchumi.

Kadhalika alilipongeza Shirika la Umoja wa Mataifa la Misaada la Marekani (USAID) kwa kazi kubwa ya kuhakikisha vijana wanatumia akili na uwezo wao kwa ajili ya kuibua kazi za miradi ya ujasiriamali ambapo mradi huo unafadhiliwa na USAID.

Ofisa mwandamizi kutoka Tume ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH), Patience Abraham, aliwataka wajasiriamali kuchangamkia fursa za ubunifu zinazopatikana katika taasisi hiyo, ili kunufaika na kupiga hatua kubwa ya maendeleo ya teknolojia na uchumi.

Alisema miongoni mwa malengo ya COSTECH ni kutumiya fursa za wajasiriamali pamoja na makundi mengine kuibuwa miradi ambayo itawawezesha kujikomboa kiuchumi.

Alisema kwa upande wa Zanzibar bado wajasiriamali hawajazitumia vizuri fursa za kazi za ubunifu kwa ajili ya kupata fedha zitakazozalisha kazi zao.

Baadhi ya washiriki wa mafunzo hayo waliwataka vijana kuchangamkia fursa zilizopo ambazo bado hazijatumika kikamilifu katika kuleta mageuzi makubwa ya kiuchumi.

Ofisa kutoka ZEEA, Raya Ahmada, alisema serikali imeanzisha taasisi hiyo kwa ajili ya kusimamia shughuli za wajasirimali na kuona wanapiga hatua kubwa ya maendeleo.

# Tanzania, Kenya zakubaliana kutatua vikwazo kibiashara

**Na Joseph Mwendapole**

TANZANIA na Kenya zimekubaliana kuendelea kutatua vikwazo vya kibiashara visivyo vya kiushuru na kuwezesha biashara ya mpakani kufanyika kwa saa 24.

Pia, zimekubaliana kuwa na mpango wa pamoja wa kuwianisha tozo, ada, ushuru na sheria zinazoathiri biasharabaina na kuondoa masharti mengine yanayoathiri biashara.

Hayo yalisemwa mwishoni mwa wiki na Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Stephen Byabato, akiwa na Waziri wa Uwekezaji, Biashara na Viwanda wa Kenya, Rebbecca Miano.

Aliyasema hayo baada ya kusaini na kukabidhiana tamko la pamoja la makubaliano (Communique), wakati wa mkutano wa nane wa kamati ya pamoja ya biashara baina ya Tanzania na Kenya ngazi ya mawaziri uliofanyika Kisumu Kenya.

Aidha, Byabato alibainisha kuwa nchi hizo zimekubaliana kuwa sheria za Tanzania hazizuii wafanyabiashara wa Kenya kufanya biashara Tanzania na Sheria za Kenya hazizuii wafanyabiashara wa Tanzania kufanya biashara nchini Kenya.

Kuhusu makubaliano yaliyotiwa saini, Byabato alisema mkutano huo uliambiwa kuwa hivi karibuni baadhi ya vikwazo visivyo vya kiushuru viliondolewa ili kukuza biashara na uchumi.

Alisema hayo yalifanyika ili kuimarisha uhusiano na Kenya ambayo ni mshirika muhimu wa kibiashara wa Tanzania.

Alisema vikwazo hivyo ni pamoja na kuondolewa kwa zuio la kuingiza chai nchini kutoka Kenya, kuondolewa kwa zuio la kuingiza Konyagi Kenya, kuondolewa kwa zuio la kusafirisha mbao kwenda Kenya kupitia mpaka wa Horohoro uliokuwa umezuliwa na Shirika la Viwango nchini Kenya.

Naye Waziri wa Uwekezaji, Biashara na Viwanda wa Kenya, Rebbecca Miano, alisema Kenya iko tayari kuendelea kushirikiana na Tanzania katika kuondoa vikwazo vya kibiashara visivyo vya kiushuru ili kukuza biashara pamoja na kuimarisha umoja wa wananchi wa nchi zote mbili.

Aidha, alisema nchi hizo mbili zimekubaliana kushughulikia baadhi ya vikwazo kwa njia za kiutendaji na kuimarisha utaratibu wa kufuatilia utekelezaji wa makubaliano na kubadilishana taarifa kuhusu maeneo ya ushirikiano wa nchi hizo.

Mkutano huo wa nane ni utekelezaji wa maagizo ya Rais Samia Suluhu Hassan na Rais William Ruto yaliyolenga kuondoa vikwazo vyote vinavyoathiri biashara ili kuimarisha uhusiano wa kibiashara.

Pia, ulilenga kushughulikia vikwazo vilivyobaki katika Mkutano wa Saba wa Biashara baina ya nchi hizo uliofanyika Machi 9-12, mwaka 2022 Zanzibar.

Mwingine unatarajiwa kufanyika Julai mwaka huu ukilenga kupunguza au kuondoa kabisa vikwazo vilivyobaki kama sehemu ya kukuza biashara na uchumi wa nchi zote mbili.



Mkurugenzi wa Mikopo wa NBC Salehe Mohammed (kulia) akiwaongoza wageni waalikwa akiwemo mgeni rasmi Katibu Mkuu wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Ally Senga Gugu (katikati) kupata chakula wakati wa hafla ya futari iliyoandaliwa na benki hiyo kwa ajili ya wateja wake jijini Dodoma. Hafla hiyo ilifanyika mwishoni mwa wiki jijini humo na kuhudhuriwa na wageni mbalimbali wakiwemo viongozi wa serikali viongozi wa dini, wateja, mawakala pamoja na wafanyakazi wa benki hiyo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mradi wa maji Mto Pangani kupeleka miji minne

**Na Steven William,** MUHEZA

SHILINGI bil. 170 zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa mradi mkubwa wa kuyatoa maji ya Mto Pangani kuyapeleka katika miji minne mkoani Tanga.

Waziri wa Maji, ambaye ni Mbunge wa Jimbo la Pangani, Jumaa Aweso, alisema hayo katika kijiji cha Mkuzi wilayani Muheza na kuelezea utekelezaji wa mradi wa maji wa miji 28, wilaya hiyo ikiwa miongoni mwa wanufaika wa mradi huo.

Alisema maji ya Mto Pangani yapelekwa kwenye mji wa Korogwe, Handeni, Muheza na Pangani ili kumaliza tatizo la maji.

Alisema vifaa vya kazi hiyo ikiwamo mabomba makubwa tayari viko katika eneo la mradi tayari kwa kuanza kazi hiyo.

"Mkipita mtayaona pale mabomba nataka nielekeze kabla maji hayo hayajafika Pangani wananchi wa kata ya Mkuzi wilayani Muheza waanze kufaidika na mradi huo kwa kupatiwa maji.

"Nataka niwaambie ndugu zangu wana Mkuzi, kama mlikuwa na changamoto ya maji, Rais Dk. Samia Suluhu Hasan, anajenga mradi mkubwa wa Sh. 170,000,000,000, leo kazi inaendelea na wakandarasi wako kazini," alisema Aweso.

Naibu Waziri wa Utamaduni Sanaa na Michezo na Mbunge wa Jimbo la Muheza, Hamisi Mwinjuma, alisema utekelezaji wa mradi wa maji wa miji 28, Muheza ni miongoni mwa wanufaika wa mradi huo mkubwa.

Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Muheza, Laick Gugu, Katibu wa CCM, Wilaya ya Muheza Simon Leng'ese, Mkuu wa wilaya, Zainabu Abdallah, Mwenyekiti wa Halmashauri, Erasto Mhina na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Muheza, Dk. Jumaa Mhina kwa nyakati tofauti walimpongeza Rais Samia kwa kuleta fedha za miradi mingi ya maendeleo ukiwamo wa maji.

# Wakwepa kifungo cha miaka 2 kwa kulipa faini

**Na Joctan Ngelly,** KAGERA

MAHAKAMA ya Wilaya Muleba, Mkoa wa Kagera imewahukumu watu wawili kutumikia kifungo cha miaka miwili jela au faini ya Shilingi milioni moja kwa kosa la ununuzi hewa wa vifaa vya kujifunzia vya Chuo cha Mafunzo ya Ufundi (VETA) Ndolage, vyenye thamani ya Sh. 2,800,000.

Washtakiwa hao ni Masanja Igorola (34), Ofisa Ununuzi Msaidizi wa Chuo cha Mafunzo ya Ufundi (VETA) Ndolage, Wilaya ya Muleba na Denis Lwegalulila (46), Mzabuni.

Washtakiwa wote walipandishwa kizimbani mbele ya Hakimu Mkazi wa mahakama hiyo, Liliani Mwambeleko na waliposomewa shtaka lao wote kwa pamoja walikiri kuhusika na kosa hilo.

Hakimu Mkazi Mwambeleko alimwambia Wakili Kiongozi wa TAKUKURU, Mkoa wa Kagera awasomee washtakiwa hao maelezo ya awali.

Wakili Kiongozi wa TAKUKURU Mkoa wa Kagera, Kelvin Murusuri, alidai kuwa, kati mwezi Agosti mwaka 2019 katika Wilaya ya Muleba, Mkoa wa Kagera, washtakiwa walifanya ununuzi hewa wa vifaa vya kujifunzia vya chuo cha VETA na kudai kuwa vimenunuliwa na kuletwa wakati sio kweli.

Murusuri aliendelea kudai kuwa Ofisa Ununuzi Msaidizi na Mzabuni walijipatia manufaa yasiyo stahiki kwa ununuzi hewa na kwamba Sh. 2,800,000 zililipwa kwa mzabuni bila kuleta vifaa husika.

Hakimu Mwambeleko aliwauliza washtakiwa kama wanakubaliana na maelezo hayo na wote walikiri.

Hakimu Mwambeleko alisema washtakiwa wote wametiwa hatiani kwa kosa hilo, pia mahakama imewataka washtakiwa kutoa utetezi wao ili waweze kupunguziwa adhabu. Washtakiwa wote waliomba kupunguziwa adhabu, kwa kuwa wana familia zinazo wategemea.

Upande wa mashtaka ukiongozwa na Wakili Kiongozi wa uliomba mahakama iwape washtakiwa adhabu kali ili iwe fundisho kwao na wengine pamoja na wazabuni wanaoendekeza vitendo vya rushwa katika ununuzi na kuitia hasara serikali.

Pia, Murusuri aliomba mahakama iliwaamru washtakiwa wote kwa pamoja kurejesha Sh. 2,800,000 zilizolipwa kwa ununuzi hewa.

Hakimu Mwambeleko alisema amezingatia maombi ya pande zote mbili na kuwahukumu washtakiwa kutumikia kifungo cha miaka miwili jela au kulipa faini ya Shilingi milioni moja ili iwe fundisho.

HABARI KIMATAIFA/KITAIFA

## Mongela ataka mgombea mmoja nafasi ya urais

**Na Elizabeth Zaya**

MWANASIASA mkongwe, Getrude Mongela, amesema katika uchaguzi mkuu 2025, hakuna haja ya kusimama mgombea mwingine katika kiny`ang`ayiro cha nafasi ya urais kwa kuwa tayari yupo Rais Samia Suluhu Hassan.

Aliyasema hayo juzi usiku kwenye hafla ya kilele cha tuzo za Malkia wa Nguvu zilizoendeshwa na Clouds Media Group, jijini Dar es Salaam na Mongela kutunukiwa tuzo ya heshima.

Alisema kama kuna mtu ana nia ya kugombea nafasi hiyo, ni vema akasubiri wakati mwingine atakapomaliza Rais Samia.

"Mimi ninakwenda kifua mbele kwa sababu sasa naona nchi yangu inatekeleza yale ambayo niliyataka. Mwaka 2025 huu mchezo wa kubabaishana babaishana na kutafutana maneno hatuhitaji sisi, watu tuko kwenye amani, mwacheni mama Samia afanye kazi yake kwa amani na nyie mkitaka subirini miaka ijayo," alisema Mongela.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, Prof. Kitila Mkumbo ambaye alikuwa mgeni rasmi katika usiku wa tuzo za Malkia wa Nguvu, aliunga mkono kauli hiyo akitamka kwamba katika nafasi ya Rais kwenye uchaguzi mkuu ujao kazi ilishaisha na maeneo ya kufanya uchaguzi ni ya wabunge na madiwani pekee.

Akizungumzia nafasi ya mwanamke kwenye uongozi, Prof. Mkumbo alisema endapo dunia ingekuwa na nusu ya viongozi, ingekuwa bora zaidi ya ilivyo sasa.

Prof. Mkumbo alisema ni lazima kumwinua mwanamke kama watu wanataka dunia iwe bora zaidi.

Alisema siri kubwa inayochangia wanaume kupata nafasi kubwa ya uongozi na kuwazidi wanawake ni kutokana na kujiweka 'kimbelembele na kiherehere' ambacho kwa wanawake imekuwa vigumu kwao.

"Wanawake wana uwezo mkubwa wa kuwa viongozi na watakuwa vizuri zaidi endapo wataongeza kimbelembele na kiherehere kidogo, sisi wanaume tunacho na ndicho ambacho tumewazidi," alisema.

Tuzo hizo za Malkia wa Nguvu zimetolewa kwa miaka minane mfululizo na Clouds Media Group, na mwaka huu zilitolewa katika vipengele tisa ikiwamo sekta ya afya, elimu, ubunifu na huduma za jamii.

Wengine waliopata tuzo hiyo ni mwandishi wa habari mkongwe, Edda Sanga, aliyetunukiwa tuzo ya Funguo ya Maisha kutokana na mchango mkubwa alioufanya katika tasnia hiyo.

# Uchaguzi uliokumbwa na vikwazo Senegal wafanyika

**DAKAR,** Senegal

WANANCHI wa Senegal hatimae wamefanya uchaguzi wa urais baada ya sarakasi za majuma kadhaa yaliyoshuhudia machafuko kutokana na tamko la kiongozi wa taifa hilo la kuahirishwa uchaguzi huo.

Ilielezwa kuwa katika uchaguzi huo watu milioni 7.3 walipiga kura kuamua kati ya wagombea 17 ambao wako kwenye kinyang'anyiro cha kumrithi Rais wa Senegal Macky Sall, ambaye ameongoza nchi hiyo tangu mwaka 2012.

Awali uchaguzi huo ulipangwa kufanyika Februari 25, lakini uliahirishwa kutokana na mzozo mkubwa wa kisiasa. Ilielezwa kuwa wananchi walishiriki zoezi hilo kuanzia saa 2:00 asubuhi vituo vya kupigia kura vilipofunguliwa hadi saa 12 jioni.

**Vile vile, ilielezwa kuwa katika tukio la duru ya pili itaandaliwa Jumapili ya pili baada ya Baraza la Katiba kutangaza matokeo ya mwisho ya duru ya kwanza.**

Aidha, uchaguzi huo unatarajiwa kumchagua rais wa tano wa Senegal, baada ya watangulizi waliopita wakiwamo Leopold Senghor aliyeongoza kuanzia (1960-1980), Abdou Diouf (1981-2000), Abdoulaye Wade (2000-2012) na Macky Sall (2012-2024) ambaye anamaliza muhula wa uongozi wake Aprili 2, mwaka huu.

Pia ilibainishwa kuwa wagombea wanaoshiriki kinyang'anyiro hicho kumrithi Rais Sall, ni Amadou Camara, Aliou Dia, Mamadou Diallo, El Hadji Diao, Mahammed Dionne, Dethie Fall, Papa Fall, Bassirou Faye, El Hadji Gakou, Serigne Mboup, Daouda Ndiaye, Aly Ndiaye, Anta Ngom, Khalifa Sall, Thierno Sall na Idrissa Seck.

Hata hivyo, ilielezwa kuwa vituo 16,440 vya kupigia kura vilifunguliwa, pamoja na 807 vya nje ya nchi. Na kwamba matokeo ya muda ya duru hiyo ya kwanza yatatangazwa kabla ya Ijumaa Machi 29, mwaka huu.

Vile vile, ilielezwa kuwa katika tukio la duru ya pili itaandaliwa Jumapili ya pili baada ya Baraza la Katiba kutangaza matokeo ya mwisho ya duru ya kwanza.

Uchaguzi huo ulikumbwa na migogoro mingi baada ya awali bunge kupanga kufanyika uchaguzi Desemba 15, mwaka huu, jambo lililokataliwa na Baraza la Katiba, pamoja na kusababisha maandamano yaliyozua taharuki nchini humo. **RFI**




Mwananchi raia wa Senegal akipiga kura katika uchaguzi wa kumchagua rais uliofanyika jana nchini humo. **PICHA: MTANDAO**

# Vifo vyafikia 133 shambulio la bomu Russia

**MOSCOW,** Russia



WATU waliofariki katika shambulio Russia wamefikia 133 huku Rais Vladimir Putin akibainisha kuwa maofisa wamewakamata watu 11 wanaodaiwa kuhusika katika uvamizi huo ambao ulisababisha uharibifu mkubwa.

Shambulizi hilo lilitekelezwa mwishoni mwa juma lililopita baada ya watu waliojificha sura kuvamia jengo lilipokuwa likifanyika tamasha na kufyatua risasi hovyo jambo lililosababisha pia zaidi ya watu 140 kujeruhiwa.

Mamlaka nchini humo ilisema watu hao 11 walizuiliwa kwa jumla, na watu wanne wenye silaha walikamatwa wakielekea Ukraine.

Katika hotuba yake kwa taifa, Rais Putin aliliita tukio hilo kuwa ni kitendo cha umwagaji damu cha kikatili na kigaidi, akisema watu wote wanne waliohusika moja kwa moja wamekamatwa.

Alisema kuwa walikuwa wakijaribu kuvuka mpaka na kuingia Ukraine taifa analolishutumu kwamba lilijaribu kubuni njia ili kuwasaidia watu hao kutoroka.

Aidha, Ukraine imekanusha vikali kuhusika na shambulio hilo. Huku Rais Putin akisema kuwa hatua za ziada za kiusalama zimewekwa kote nchini humo na kutangaza Machi 24 jana, kuwa siku ya maombolezo ya kitaifa.

Hata hivyo, tawi la kundi la Islamic State nchini Afghanistan lilidai kuhusika na shambulio hilo la Ijumaa katika taarifa iliyowekwa kwenye mitandao ya kijamii.

Ofisa wa ujasusi wa Marekani aliliambia shirika la habari la Associated Press kwamba mashirika ya Marekani yamethibitisha kuwa kundi hilo lilihusika na shambulio hilo. **VOA**

HABARI MICHEZO

# KATIBU TWFA AWATAKA MWFA KUWEKEZA SOKA LA VIJANA

**Na Mwandishi Wetu,** Morogoro

KATIBU Mkuu wa Chama cha Mpira wa Miguu cha Wanawake nchini (TWFA), Somoe Ng'itu, amewataka viongozi wa chama hicho ngazi za wilaya na mikoa kuwekeza katika soka la vijana kwa kuanzisha mashindano ili kuibua vipaji vya wachezaji watakaodumu kwa muda mrefu kimichezo.

**Somoe aliyasema hayo mjini Morogoro wakati akifungua Mkutano Mkuu wa Chama cha Mpira wa Miguu cha Wanawake Mkoa wa Morogoro (MWFA), ambapo alihimiza ushirikiano miongoni mwa viongozi na wadau wa soka ili kuinua mchezo huo kwa wanawake.**

Alisema kwa kuanzisha timu za vijana na watoto chini ya ya umri wa miaka 21, 17 na 14, kutasaidia kuwa na timu imara zitakazocheza na kushindana katika michuano mbalimbali ndani na nje ya Tanzania.

Katibu Mkuu huyo wa TWFA, ambaye pia ni Kamishna wa Michezo wa Shirikisho la Soka barani Afrika (CAF), aliwahimiza pia viongozi wa soka la wanawake kuanzisha utaratibu wa kuwapata watoto wa kike wanaopenda mpira kuanzia ngazi ya chekechea na shule za msingi ili kutengeneza timu nzuri za wanawake kuanzia ngazi za chini.

Kuhusu ushirikiano, alisema ni vema viongozi na wadau wa soka kushirikiana ili kuendeleza soka la wanawake ambalo limekuwa na fursa hususan ni ajira.

"Mahali popote penye mshikamano na upendo huwa wafadhili wanajitokeza na kusaidia, lakini kama hakuna ushirikiano hakuna mdau atakayejitokeza kusaidia timu. Sikilizeni ushauri wa wadau, fuateni katiba na maelekezo ya TWFA na MWFA, lakini pia ya TFF na MRFA ili msonge mbele kwa manufaa ya mpira wa wanawake," alisisitiza Somoe.

Kwa upande wa Mwenyekiti wa MWFA, Beatrice Selemani, alisema chama hicho kimedhamiria kuweka mazingira mazuri ya kuchezwa mpira wa miguu kwa wanawake mkoa mzima na kuimarisha utendaji kazi wenye weledi katika ngazi zote.

Alisema katika kuhakikisha kiwango cha soka la wanawake kinainuliwa ni lazima ushirikishwaji uwapo katika ngazi zote za uongozi na utawala na MWFA kwa kushirikiana na wadau wa soka ni lazima wakae pamoja kujadili kwa kina mchezo huo ambao umeshika kasi kubwa na kutoa ajira kwa watoto wa kike nchini.

"Tunatoa wito kwa wadau mbalimbali kujitokeza ili kuunga mkono uendeshaji wa soka la wanawake Mkoa wa Morogoro, mwaka huu tumejipanga na kuelekeza nguvu zaidi kuhakikisha soka la wanawake linachezwa kila wilaya, kutoa elimu na mafunzo kwa viongozi wa vyama vya wilaya vya soka la wanawake na kuzalisha walimu wa soka wenye taaluma ya kutosha," alisema.

Naye Mjumbe wa Mkutano Mkuu Taifa wa TWFA akiwakilisha Mkoa wa Morogoro, Idda Mushi, aliwahimiza wachezaji wa kike kulinda nafasi yao ya uanamke wakishiriki michezo ili kutopoteza uhalisia wao.

"Kama unasuka basi suka, kama unabana nywele bana, kucheza mpira hakukufanyi ubadili jinsia uwe mwanaume, uvae na kutembea kama mwanaume, unyoe kama mwanaume, lindeni uhalisia wenu kama wanawake," alisema Idda.

Aidha, Mwenyekiti wa Chama cha Mpira wa Miguu Mkoa wa Morogoro (MRFA), Paschal Kihanga, alihimiza mafunzo zaidi kutolewa kwa walimu wa soka ili wasaidie kufundisha kwa kuwa viongozi peke yao na wachezaji bila makocha haitasaidia kuendeleza mpira wa miguu.



Katibu Mkuu wa Chama cha Mpira wa Miguu cha Wanawake Tanzania (TWFA), Somoe Ng'itu, akifungua mkutano mkuu wa Chama cha Soka cha Wanawake Mkoa wa Morogoro (MWFA), uliofanyika mkoani humo juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# *Ngumi DABA kuanza kupigwa Mbezi leo*

**Na Shufaa Lyimo**

MASHINDANO ya wazi ya ngumi Mkoa wa Dar es Salaam yanatarajiwa kuanza kunguruma leo Machi 25 hadi 31, mwaka huu kwenye Ukumbi wa Klabu ya FM uliyopo Mbezi, Kimara Dar es Salaam.

Akizungumza na Nipashe jana, Mwenyekiti wa Chama cha Ngumi Mkoa wa Dar es Salaam (DABA), Akalory Godfrey, alisema kabla ya mashindano hayo wataanza na zoezi la kupima uzito litakalofanyika asubuhi.

Alisema maandalizi yamekamilika kwani wamejipanga vema kuhakikisha yanafanyika kwa weledi na kupata walichokikusudia.

"Kwa kuwa walengwa ni watoto wenye umri wa miaka 15, 16, na 17 pamoja na vijana wenye miaka 18 wa jinsi zote, hili tutalizingatia tukiwa na lengo la kutengeneza vipaji vya mkoa na taifa," alisema Godfrey.

Alisema lengo ni kutoa fursa kwa watoto kuonyesha vipaji vyao pamoja na kupata timu za vijana wenye umri huo kwani wataandaliwa kwa ajili ya mashindano mbalimbali ya kitaifa.

Aidha, alisema kuwa mashindano hayo yatachezwa kwa mtindo wa ligi ili kutoa nafasi ya wachezaji kushiriki mapambano mengi na kupata bingwa.

Mwenyekiti huyo alisema milango ipo wazi kwa wadau wa michezo na wadhamini kuja kuwashika mkono kufanikisha mashindano hayo na kuibua vipaji.

## Dodoma Jiji FC yataja mechi 10 za hatari kwao

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Dodoma Jiji imetangaza mechi 10 ambazo zimesaliwa kwao kabla ya kuhitimisha Ligi Kuu msimu huu, kwao ni fainali na mkakati wao ni kushinda zote ili kusalia katika ligi hiyo msimu ujao.

Mechi 10 ambazo imesaliwa nazo ni dhidi ya Kagera Sugar, Singida Fountan Gate, Ihefu, Mashujaa na Simba ambazo itacheza ugenini, za nyumbani ni dhidi ya JKT Tanzania, KMC, Prisons, Namungo, na Yanga.

Kocha Mkuu wa timu hiyo, Francis Baraza, amesema sehemu waliopo kwenye msimamo wa ligi si salama na inatia hofu, hivyo mkakati wao ni kuzifanya mechi hizo 10 zilizosalia kuwa kama fainali, kwa lengo la kushinda zote na kubaki Ligi Kuu.

"Wachezaji wameanza mazoezi, kasoro Emmanuel Martin na Mohamed Hussein, kusema kweli ligi ni ngumu na nafasi yetu inatia hofu. Sehemu tuliopo si salama, nimeanza kutengeneza mkakati wa kuhakikisha tunashinda mechi zote za nyumbani na ugenini, kwa sababu zote zilizosalia tunatakiwa kucheza kama fainali ili kushinda, tuna uwezo huo, vijana wana uwezo wa kufanya hivyo," alisema Baraza.

## Kengold, Pamba zang'ang'aniana

**Na Adam Fungamwango**

TIMU za Kengold na Pamba juzi ziling'ang'aniana kooni na kutoka sare ya mabao 2-2 katika mechi ya raundi ya 26 ya Ligi ya Championship, kila moja ikijiongezea pointi moja katika kusaka nafasi ya kupanda moja kwa moja Ligi Kuu Tanzania bara msimu ujao.

Katika mechi hiyo kali iliyopigwa Uwanja wa Sokoine, Mbeya, wenyeji, Kengold walipata mabao yao mawili kupitia kwa Edger William, mabao ya Pamba yakifungwa na winga wa zamani wa Simba, Haruna Chanongo.

Wakati matokeo hayo yakiinufaisha zaidi Kengold, ikiwa imefikisha pointi 60 kileleni mwa msimamo, ikiwa kwenye hatua chache tu za kupanda Ligi Kuu Tanzania Bara kwa msimu ujao ikibakiwa na mechi nne tu, yamewafanya Pamba kuwa kwenye wakati mgumu, kwani imefikisha pointi 55 ambazo zinaweza kupitwa na Biashara United kwani kama ikishinda mechi ijayo itafikisha alama 56.

Zikiwa zimebaki raundi nne tu kabla ya kutamatika kwa Ligi ya Championship, inaonekana vita kubwa ipo baina ya Pamba na Biashara United kusaka nafasi moja ya kupanda moja kwa moja Ligi Kuu bila kwenda kwenye 'play off.'

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### TEN HAG APAMBANA KUBAKI

KOCHA wa Manchester United, Erik ten Hag, anaamini kuwa bado ana muda wa kumshawishi mmiliki mwenza wa klabu hiyo, Sir Jim Ratcliffe, kuendelea naye, licha ya majadiliano kufanyika kuhusu mrithi wake. ***(ESPN)***

### DIOMANDE, INACIO WATAKWA

NEWCASTLE United inataka kumsajili beki wa kati wa Ureno, Goncalo Inacio mwenye umri wa miaka 22, na mlinzi wa Ivory Coast, Ousmane Diomande (20), kutoka Sporting Lisbon, lakini vikwazo vya kifedha vinaweza kuwazuia. ***(Fichajes)***

### CUBARSI MKATABA MPYA

BARCELONA ina nia ya kumpa mkataba mpya mlinzi Pau Cubarsi mwenye umri wa miaka 17, baada ya mafanikio yake katika kikosi cha kwanza, huku kukiwa na nia kutoka Ligi Kuu England. ***(Marca)***

### GIBBS-WHITE AFUATILIWA

ARSENAL inamfuatilia kiungo wa kati wa England, Morgan Gibbs-White, 24, huku Nottingham Forest ikifikiria kumuuza mchezaji huyo ili kusawazisha vitabu vyao vya kuuza na kununua. ***(Star)***

### YAMAL HAYUPO SOKONI

RAIS wa Barcelona, Joan Laporta, amesema klabu hiyo ilikataa ofa ya euro milioni 200 kwa mshambuliaji wa Hispania, Lamine Yamal, 16. ***(Marca)***

### RAPHINHA ATAKIWA SAUDIA

KLABU ya Saudi Arabia ya Al-Hilal inataka kumnunua winga wa Brazil, Raphinha, 27, kutoka Barcelona na iko tayari kutoa ofa ya hadi euro milioni 100 kwa mchezaji huyo. ***(Sport)***

### MBAPPE HATATANGAZA

FOWADI wa Ufaransa, Kylian Mbappe hatatangaza kuhama kwake kutoka Paris St-Germain kwenda Real Madrid hadi kila kitu kitakapokuwa sawa. ***(Sport)***

### GREENWOOD ATAKIWA JUVE

JUVENTUS inataka kumnunua fowadi, Mason Greenwood, 22, ambaye yuko kwa mkopo Getafe kutoka Manchester United na ambaye mkataba wake na klabu hiyo ya Old Trafford utakamilika mwaka 2025. ***(Gazzetta dello Sport)***

### FRANKFURT NA DE BEEK

KLABU ya Eintracht Frankfurt haina uwezekano wa kutumia kipengele cha pauni milioni 8.5 ili kumsajili moja kwa moja kiungo wa kati wa Uholanzi, Donny van de Beek, 26, kutoka Manchester United. ***(Bild, via Goal)***

### AMRABAT HATABAKISHWA

KLABU ya Manchester United haitatafuta kumsajili mchezaji aliyecheza kwa mkopo kutoka Fiorentina, Sofyan Amrabat, 27, lakini kiungo huyo wa kati wa Morocco analengwa na AC Milan na Juventus. ***(Tuttosport via Football Italia)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# KANE SASA AREJESHWE RASMI BAYERN KUTIBIWA

**LONDON,** England

### ●●● Amerudi, hatakuwa sawa kwa mchezo wa kesho Wembley dhidi ya Ubelgiji...

MSHAMBULIAJI wa England, Harry Kane, amerudishwa Bayern Munich ili kuendelea kupata nafuu kutokana na jeraha la kifundo cha mguu, Kocha wa England, Gareth Southgate, amethibitisha.

**Kane hatacheza mchezo wa kirafiki wa kimataifa dhidi ya Ubelgiji kwenye Uwanja wa Wembley kesho Jumanne.**

Kane alijiunga na kikosi cha England kabla ya mechi ya kirafiki dhidi ya Brazil licha ya kupata jeraha la kifundo cha mguu wakati Bayern iliposhinda mabao 5-2 dhidi ya Darmstadt wiki moja iliyopita.

Alikuwa jukwaani wakati England ikichapwa bao 1-0 na Brazil Jumamosi, na baadaye Southgate alithibitisha kuwa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 30, atarejea Ujerumani kwa matibabu na hatakuwa sehemu ya mchezo dhidi ya Ubelgiji.

Bayern itacheza na Borussia Dortmund kwenye Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga, Jumamosi na baadaye kucheza dhidi ya Arsenal kwenye robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya baadaye Aprili 9, mwaka huu.

"Anarudi, hatakuwa sawa kwa mchezo wa Jumanne," alisema Southgate alipotangaza katika mkutano na waaandishi wa habari.

Kwa kukosekana kwa Kane, England iliangukia kwenye kichapo dhidi ya Brazil, ambao walishinda kutokana na bao la kwanza la kimataifa la Endrick mwenye umri wa miaka 17.

Kinda huyo, ambaye anatazamiwa kujiunga na Real Madrid majira ya joto, aliingia akitokea benchi kipindi cha pili na kutumia vema shuti la Vinicius Junior lililookolewa na Jordan Pickford na kumkuta mfungaji huyo mwenye umri mdogo zaidi katika dimba la Wembley.

"Tunafahamu ni mchezaji hatari na amefuata bao," alisema Southgate.

"Tulipaswa kulinda bao vizuri zaidi kuliko tulivyolinda, lakini ni wakati mzuri kwake."

Ulikuwa usiku wa kusikitisha kwa England, ambao wana mechi tatu pekee kabla ya kuelekea Ujerumani kwa ajili ya michuano ya Ulaya msimu huu.

Brazil, waolijumuisha wachezaji 11 ambao hawakuwa kwenye kikosi chao, walipata nafasi nzuri zaidi lakini Southgate, ambaye alimchezesha kwa mara ya kwanza kijana wa Manchester United Kobbie Mainoo katika kipindi cha pili, alisisitiza kwamba "alifurahishwa" na uchezaji wao.

"Kwa kweli hatupendi kupoteza, lakini nilifikiri kulikuwa na uchezaji mzuri sana kutoka kwa wachezaji ambao hawajaichezea England," alisema Southgate.

"Tumekuwa na majaribio mengi kwenye goli kama wao, lakini tofauti ilikuwa wakati mmoja na huo ni ukatili wa mpira wa miguu katika kiwango hiki.

"Unashughulika na wachezaji wa hali ya juu na utakuwa na wakati ambapo kipa wako atalazimika kuokoa. Nilidhani tulikuwa na wakati upande mwingine. Ulikuwa mchezo sawa na kama ungemalizika kama mchezaji bora.

"Kulikuwa na makosa madogo madogo na hiyo iliamua mchezo."



# ALONSO ACHAGUA WAPI PA KWENDA

**MUNICH,** Ujerumani

KOCHA wa Bayer Leverkusen, Xabi Alonso anatarajiwa kupendelea kuhamia Bayern Munich ikiwa ataamua kuondoka katika timu yake ya sasa msimu unaokuja wa majira ya joto, ripoti imedai.

Alonso amefurahia msimu mzuri akiwa na Bayern Leverkusen ambao umewaacha kwenye kilele cha kushinda Bundesliga, na uchezaji wa kikosi chake umevutia bila ya kushangaza baadhi ya wababe wa Ulaya, ambao wengi wao wanatafuta makocha wapya kabla ya msimu wa 2024/25.

Miongoni mwa wanaowania saini ya Alonso ni Bayern na Liverpool, wote waajiri wa zamani wa raia huyo wa Hispania wakati wa enzi zake za kucheza, lakini Florian Plettenberg wa Sky Germany anaamini Alonso atajiunga na Bayern ikiwa ataamua kuondoka msimu huu wa majira ya joto.

Wakati kuondoka kwa Alonso kutoka Leverkusen kwa sasa ni mbali na uhakika, inasemekana kwamba kiungo huyo angechagua kujiunga na Bayern mbele ya Liverpool ikiwa ataamua kubadili klabu katika miezi ijayo.

Mazungumzo rasmi bado hayajafanyika, lakini maofisa wa Bayern wanaamini Alonso ameamua na angependelea kuhamia Munich.

Mkataba wa Alonso na Leverkusen utaendelea hadi 2026, lakini nahodha wa klabu hiyo, Lukas Hradecky hivi majuzi alikiri kwamba hakuna mtu kwenye chumba cha kubadilishia nguo ambaye atamlaumu bosi huyo ikiwa atachagua kuchukua hatua nyingine katika maisha yake ya soka msimu huu wa majira ya joto.

"Hayo ni matakwa na ndoto yetu yeye kubaki, lakini hakuna atakayekasirika au kubishana ikiwa atashinda Bundesliga na kuamua kwenda njia nyingine," alisema Hradecky.

# Araujo akanusha kuondoka Barcelona

**BARCELONA,** Hispania

MLINZI wa kati wa Barcelona, Ronald Araujo, amesisitiza kuwa bado ana furaha katika klabu hiyo, akipuuza ripoti kwamba anaweza kuondoka msimu huu wa majira ya joto.

Wakati Araujo akibakia kuwa mchezaji muhimu wa Barcelona, imependekezwa kuwa anaweza kuuzwa msimu huu wa majira ya joto ili kukusanya kiasi kikubwa cha fedha, huku timu kama Bayern Munich na Manchester United zikipigiwa upatu kuwasilisha ombi la kumnunua mchezaji huyo wa Kimataifa wa Uruguay.

Hata hivyo, Araujo ameamua kuweka uvumi huo wazi, akisisitiza furaha yake na maisha ya Barcelona.

"Kumekuwa na mazungumzo mengi kuhusu hili, lakini nina furaha Barcelona," alisema akiiambia La Quinta Tribuna.

"Mbali na hilo, tunapaswa kumaliza msimu vizuri kwa sababu bado kuna changamoto mbeleni, ikiwa ni pamoja na Copa America."

Kinachochochea moto wa uwezekano wa kuondoka ni ukweli kwamba mkataba wa sasa wa Araujo unatarajiwa kumalizika 2026 na huenda Barcelona wasiweze kushindana na aina ya mishahara ambayo atapewa kwingineko.

Rais wa Klabu Joan Laporta, ambaye hapo awali alikiri kuwa atamfunga Araujo kwa mkataba wa maisha ikiwezekana, hivi karibuni alikiri kumekuwa na vikwazo katika mazungumzo na wawakilishi wa beki huyo wa kati, lakini akasisitiza masuala yote sasa yameshughulikiwa.





# Endrick aweka rekodi Wembley

**LONDON,** England

ENDRICK alikua mfungaji mwenye umri mdogo zaidi kuwahi kufunga katika mchezo wa timu ya wakubwa kwenye Uwanja wa Wembley wakati Brazil ilipoibuka na ushindi wa dakika za lala salama wa bao 1-0 dhidi ya England Jumamosi usiku.

Fowadi huyo wa Palmeiras alivunja rekodi hiyo akiwa na umri wa miaka 17 na siku 246, akifunga bao lake la kwanza akiwa na Brazil katika mchakato huo na kuhitimisha mfululizo wa mechi 21 za England bila kufungwa kwenye uwanja huo.

Endrick, ambaye atajiunga na Real Madrid Julai, alifunga bao hilo kwa utulivu mkubwa Kaskazini-Magharibi mwa London.

Andreas Pereira alimtengenezea Vinicius Junior pasi nzuri baada ya Lewis Dunk kukimbia na mpira mbele, na winga huyo alielekeza kombora la chini chini lililomlenga kipa Jordan Pickford ambaye aliutema mpira na kumkuta kinda huyo wa Brazil ambaye aliukwamisha mpira wavuni.

Endrick alizaliwa siku 12 baada ya fainali ya Kombe la Dunia la 2006 na alikuwa bado hajazaliwa wakati Zinedine Zidane alipompiga kichwa Marco Materazzi kwenye fainali hizo.

Hii ilikuwa mechi yake ya tatu tu kuichezea Brazil, lakini tayari amejijengea jina katika nchi yake akiwa ameichezea Palmeiras mara 66, akifunga mabao 18. Mchezo wa kwanza wa Endrick nchini England ulisababisha wakala wake kufichua mapema wiki hii kwamba alikaribia kusaini Chelsea badala ya Madrid.

"Nadhani Real waliamua kwamba hawatakosa kipaji hiki kama Vini au Endrick baada ya Neymar kuhamia Barcelona," alisema Frederico Pena akiliambia gazeti la Daily Telegraph.

# *Wachezaji Simba waikalia kikao Al Ahly*

**Na Adam Fungamwango**

WACHEZAJI wa Simba wamesema huu ni wakati mzuri kwao kuandika historia mpya kwenye soka la klabu hiyo na Tanzania kwa ujumla kwa kuwaondoa mashindanoni Mabingwa wa Afrika, Al Ahly ya Misri na wao kutinga hatua ya nusu fainali.

Akizungumza kwa niaba ya wachezaji wenzake kipa wa timu hiyo, Ali Salim, amesema wamekaa kikao wao kwa wao na kuambizana kuwa safari hii hakuna cha kuwazuia kwenda nusu fainali kama watapambana, kwani kiwango chao kwa sasa kinafanana kabisa na timu kubwa barani Afrika.

Salim alisema kikao chao kama wachezaji kilifanyika mara baada ya droo kufanyika, hivyo kwa sasa wanachosubiria ni siku ya mechi tu ili waonyeshe kile ambacho waliahidiana kukifanya.

"Naongea kwa niaba yao kuwa tunafanya mazoezi vizuri na tunapata muda wa kupumzika vizuri, timu tunayocheza nayo ni kubwa Afrika, tumeshawahi kucheza nayo mara kwa mara japo hatujawahi kufanya vizuri sana, kocha kasema tuje huku ili tuweze kufanya vizuri kwenye mechi inayokuja na sisi tuna imani hiyo.

"Baada ya droo kufanyika, kila mchezaji alionekana kuwa na imani ya kusonga mbele, na sisi wenyewe tukakutana na tukaambizana kuwa timu zilizoingia zote ni za levo yetu, hata hawa Al Ahly kwetu si wa kuwahofia kivile hapo wenzetu wamtupita kidogo," alisema Salim.

Alisema anaamini kuwa robo fainali ngumu zaidi waliowahi kucheza ni dhidi ya Kaizer Chiefs iliyochezwa Mei 15, 2021 waliyofungwa mabao 4-0 nchini Afrika Kusini, kabla ya kushinda mabao 3-0 Mei 22, mwaka huo jijini Dar es Salaam.

"Robo fainali ile ngumu sana, tulijisahau tukaruhusu mabao mengi ugenini, tukawa na mlima mrefu nyumbani, lakini hata maandalizi naamini hayakuwa mazuri kama tunavyojiandaa hivi sasa.

Ile ya TP Mazembe tuliyotoa sare na kufungwa mabao 4-1 ugenini tulitolewa kwa sababu ya ugeni tu wa mashindano, kipindi kile hatukuwa na utayari sana," alisema kipa huyo.

Kipa huyo alisema robo fainali iliyokuwa rahisi zaidi kwao ilikuwa ya msimu uliopita dhidi ya Wydad Casablanca, lakini makosa machache tu yaliwagharimu.

"Mechi na Wydad Casablanca kilichotufelisha ni kutoimaliza nyumbani, tungepata hata bao moja na nusu tu, achilia mbali mawili tulikuwa tunavuka, kule tulikaza wakapata moja, hatimaye mikwaju ya penalti ikaamua," alisema.

Aprili 29, 2023, Simba ilitolewa kwa penalti 4-3, baada ya timu hizo kushinda bao 1-0 nyumbani kila mmoja.

Wakati huo huo kikosi cha timu hiyo kinatarajia kurejea jijini Dar es Salaam kesho tayari kwa kuwavaa mabingwa wao.

Meneja Habari na Mawasiliano, Ahmed Ally, amesema maandalizi kuelekea mchezo huo yamekwenda kama yalivyopangwa.

"Mazingira ya kambi huwa yanatoa ujumbe kwa wachezaji, walivyoona tumekwenda Zanzibar hata wao wakaona kuwa hii mechi si ya kawaida, wamesema wako tayari kwenda kuipania Simba na wanafurahishwa na maandalizi yanayofanyika," alisema Ahmed.

# CHANGALAWE, MAREGESI WAPIGWA ALL-AFRICAN GAMES, WAPEWA MEDALI

**Na Saada Akida**

TANZANIA imejihakikishia kurejea na medali tatu kupitia mchezo wa ngumi licha ya matokeo mabaya aliyoyapata nahodha wa Timu ya Taifa ya Masumbwi, Yusuf Changalawe, baada ya kupoteza kwa pointi katika hatua ya nusu fainali dhidi ya Pita Kabeji kutoka DR Congo katika michezo ya All-African Games inayoendelea jijini Accra, Ghana.

Pambano hilo lilikuwa la uzani wa Light Heavyweight Kg 80 ambapo Changalawe alicheza kwa ustadi wa hali ya juu, lakini maamuzi ya majaji yakampa ushindi mpinzani wake, Kabeji.

**Bondia mwingine aliyeishia katika nusu fainali ni Musa Maregesi katika uzani wa Cruiserweight Kg 86 baada ya kupoteza pia katika hatua hiyo ya nusu fainali dhidi ya Kanouni O, kutoka Algeria kwa pointi 5-0.**

Katika mchezo huo wa ngumi Tanzania imejihakikishia kurejea na medali tatu za shaba kutoka kwa Changalawe, Maregesi na Ezra Paulo.

Kwa mujibu wa Rais wa Shirikisho la Ngumi Tanzania, Lukelo Willilo, huo ni mwanzo mzuri wa kujivunia mafanikio hayo kwa kuanzia 2024 na kuendelea pale walipoishia mwaka jana.

"Huu ni mwanzo mzuri kwetu Watanzania kwa kuanza mwaka 2024 kwa kupata medali ya shaba. Ni mwanzo mzuri na tunaona jinsi ambavyo tunaweza kuendelea kwenye mashindano yajayo kuendeleza pale wanapoishia," alisema Lukelo.

Mchezo wa ngumi mwaka 2023 ulieletea nchi medali tatu kutoka katika Mashindano ya Ubingwa wa Afrika Yaounde 2023, Cameroon, moja ikiwa ya fedha ambayo aliipata Grace Mwakamele na Shaba ilikuwa kwa Changalawe alifanikiwa kupata medali nyingine ya fedha katika mashindano ya kufuzu kushiriki Olimpiki ya Paris 2024, kwa Bara la Afrika.



Wachezaji wa Taifa Stars wakiwa mazoezini nchini Azerbaijan jana kujiandaa na mechi ya Fifa Series 2024 dhidi ya Mongolia itakayopigwa leo nchini humo. **PICHA: TFF**

## Simba, Yanga robo fainali

INATOKA UKURASA 24

nchini.

Kurejea kwa wachezaji hao kumeshusha presha kwa wanachama na mashabiki wa timu hizo ambao walikuwa na wasiwasi na baadhi ya wachezaji wao tegemeo kwenye vikosi hivyo kuelekea katika mechi muhimu za robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Meneja Habari na Mawasiliano wa Klabu ya Simba, Ahmed Ally, jana alisema baada ya kuwasili alfajiri, wachezaji wao walipumzika kidogo jijini Dar es Salaam asubuhi waliwasafirisha kuelekea mjini Zanzibar kuungana na wenzao kwenye kambi ya muda kabla ya kurejea Dar kesho Jumanne.



## Stars waipania Mongolia leo

INATOKA UKURASA 24

Kibu naye alikosa bao la wazi dakika ya 20, kwa kugongeza nguzo ya pembeni, akiwa amebaki na kipa Dimitar Mitov wa Bulgaria, na Clement Mzize akigongesha mwamba wa juu katika dakika ya 90 ya mchezo kwennye mechi hiyo ambayo Stars ililala kwa bao 1-0.

# Michezo

Jumatatu Machi 25, 2024

Nipashe




Kane arejeshwe Bayern kutibiwa

UKURASA 21





Wachezaji wa Simba (kulia) na wa Yanga (kushoto), wakifanya wakiwa mazoezini. Timu hizo Ijumaa na Jumamosi zitavaana dhidi ya Al Ahly kwa Simba na Mamelodi kwa Yanga mechi zikipigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa. **PICHA: WAPIGAPICHA WETU**

# Simba, Yanga kamili kwa robo fainali CAF

**Na Adam Fungamwango**

●●● Zaiachia Stars nyota wao na kuwapokea Kibu, Tshabalala, Bacca na Mudathir...

WACHEZAJI baadhi wa timu za Simba na Yanga waliokuwa kwenye kikosi cha Timu ya Taifa ya Tanzania, Taifa Stars, wamewasili nchini tayari kujiunga na timu zao kwa mechi za robo fainali, Ligi ya Mabingwa Afrika zitakazopigwa mwishoni mwa wiki, huku wengine wakisalia Azerbaijan.

**Wachezaji wa timu hizo walikuwa ni sehemu ya kikosi cha Taifa Stars kilichokwenda nchini Azerbaijan kucheza mashindano maalum ya FIFA Series 2024 yanayoendelea.**

Ofisa Habari na Mawasiliano wa Shirikisho la Mpira wa Miguu (TFF), Cliford Ndimbo, amesema wachezaji hao walirejea alfariji ya kuamkia jana kama ambavyo ilivyokuwa makubaliano ya klabu zao na shirikisho hilo.

Kwa upande wa Simba waliorejea kuwahi maandalizi ya mechi ya robo fainali dhidi ya Al Ahly ya Misri itakayopigwa Ijumaa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, ni Kibu Denis na Mohamed Hussein 'Tshabalala', huku Clement Mzize, Ibrahim Hamad 'Bacca' na Mudathir Yahaya wakiwasili kwa upande wa Yanga ambao nao watajiunga na kambi ya timu yao kuwahi mechi ya hatua hiyo dhidi ya Mamelodi Sundowns ya Afrika Kusini Jumamosi.

"Wachezaji wamerejea alfajiri ya leo kama ilivyokuwa makubaliano yetu na klabu zao, ni kweli kuna wengine wamebaki pia kutokana na makubaliano pia, wao watakuja kujiunga na timu baada ya mechi ya pili ya Stars," alisema Ndimbo.

Wachezaji waliobaki kwa upande wa Simba ni Kennedy Juma na Aishi Manula ambaye katika mechi ya kwanza alipata majeraha, na kwa Yanga waliosalia nchini humo ni Aboutwalib Mshery na Bakari Mwamnyeto.

Wachezaji hao wanatarajiwa kuwa sehemu ya kikosi kitakachoivaa Mongolia leo na baada ya mechi hiyo nao, wataanza safari ya kurejea

INAENDELEA UKURASA 23

# Taifa Stars waipania Mongolia

**Na Adam Fungamwango**

KIKOSI cha Timu ya Taifa ya Tanzania, Taifa Stars leo kitashuka tena kwenye Uwanja wa Dalga Arena nchini Azerbaijan kucheza dhidi ya Mongolia katika mechi ya mashindano maalum ya FIFA Series 2024 yanayoendelea nchini humo.

Stars itakuwa inajaribu bahati yake baada ya mechi ya kwanza Ijumaa iliyopita kuchapwa bao 1-0 dhidi ya Bulgaria katika mfululizo wa michezo ya michuano hiyo.

Kocha Mkuu wa Stars, Hemed Suleiman 'Morocco', amewahakikishia Watanzania kuwa katika mechi ya leo wanatarajia kuibuka na ushindi kwani haiwezekani wapoteze michezo miwili mfululizo.

"Tumebakiwa na mchezo mmoja ambao ni huu, mechi iliyopita tulipoteza ila kiwango kilikuwa kizuri, kwangu mimi si kitu chenye tija kuona tunapoteza mechi zote mbili.

"Tumekaa na wachezaji tukaangalia mapungufu ya mechi ya kwanza, tumeyarekebisha, Mongolia nimeiangalia kiwango chake ni kama Bulgaria tu, tunawaheshimu, lakini tunahitaji kupata matokeo ya ushindi,tunahitaji kuongeza nguvu. tunajipanga kwenda kupambana," alisema Morocco.

Feisal Salum aliwaahidi Watazania ushindi katika mechi ya leo kwani wamefanyia kazi mapungufu yaliyojitokeza katika mechi iliyopita.

"Sisi kama wachezaji tuko vizuri, nilikosa mabao kwenye mchezo uliopita haikuwa bahati yangu, ila nawaahidi katika mchezo huu nikipata nafasi nzuri nitafunga, na nawaahidi Watanzania ushindi.

Katika mechi ya Ijumaa, Fei Toto alikuwa miongoni mwa wachezaji walioikosesha Stars mabao matatu ya wazi, ambapo alipiga juu akiwa na kipa, huku pia akiwa na uwezo wa kumpasia Kibu Denis aliyekuwa kwenye eneo zuri zaidi.

INAENDELEA UKURASA 23



9 770856 541002 >